# MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

‘Mshtakiwa alibadili nguo kabla gwaride la utambulisho’



UKURASA 5

**BoT** yasisitiza marufuku dola kutumika kulipia mahitaji nchini

UKURASA 3



Tanzania kufuta maeifu ya asasi kulivyoistua dunia

Uhalifu wa ADF Uganda unavyotishia usalama EAC

siasa

JUMATANO JUNI 21, 2023 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

WAZIRI MWIGULU NCHEMBA Anatisha jimboni anabebwa juu juu asijikwae, wapigakura wakiri amefanya maajabu Iramba

KATIBA KWA MASILAHI YA TAIFA

## Ulinzi muungano, rasilimali, maisha bora kufuta umaskini

UKURASA 11



# Nipashe

Jumatano Juni 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581348

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



BAJETI 2023/24

# Wenye viwanda wakosoa tozo 8

UKURASA 2




# Mpina ambana Mwigulu matumizi ya Tril. 2.7/-



UKURASA 2

## Kibano chaja wanaochelewa kulipa mafao ya wastaafu

UKURASA 3

**MICHEZO** MAYELE SASA AANIKA HATIMA YAKE YANGA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Dk. Samwel Shelukindo, akizungumza na Balozi wa Canada nchini, Kyle Nunas katika ofisi ndogo za wizara jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye viwanda wakosoa tozo 8

**Na Waandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda (CTI) limeorodhesha hatua kadhaa za kikodi zinazohitaji kuangaliwa upya katika utekelezaji wa bajeti ya serikali iliyopendekezwa kwa mwaka ujao wa fedha, likihadharisha zinaweza kuathiri maendeleo ya viwanda.

Katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mapendekezo ya bajeti ya serikali yaliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita, Makamu Mwenyekiti wa CTI, Hussein Sufian, aliipongeza serikali kwa kufanya mageuzi mbalimbali katika muundo wa kodi, ada, tozo na marekebisho ya sheria na kanuni ili kuboresha mazingira ya biashara.

"Hatua za kodi zinazochukuliwa na serikali zitawezesha viwanda vya ndani kupunguza gharama za uzalishaji, kuboresha ustawi wa walaji, kukuza matumizi ya vifaa vya ndani, kuongeza ushindani na ukuaji wa uchumi lakini kuna mengine ambayo yanahitaji kuangaliwa upya," alisema.

Sufiani alibainisha baadhi ya hatua za kikodi ambazo CTI inataka ziangaliwe upya ili kutoathiri viwanda na uchumi wa nchi, zikijumuisha pendekezo la kufanya marekebisho ili kutoza asilimia 10 ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa zisizo za petroli na asilimia 20 kwa bia na bidhaa za tumbaku.

Pia wanakosoa pendekezo la kuanzishwa ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha Sh. 20 kwa kilo ya saruji inayoagizwa kutoka nje na inayozalishwa nchini.

Hatua nyingine ambazo CTI inataka ziangaliwe upya ni pamoja na kuahirisha utumaji maombi wa kiwango cha asilimia 50 cha Cheti cha Forodha cha Afrika Mashariki (EAC CET) na kutoza ushuru wa asilimia 35 kwa vitenge kutoka nje.

Alisema CTI pia inaona ukakasi katika pendekezo la kupunguza uthamini wa pamba, kanga na kitenge, wakiamini kutaifanya Tanzania kuwa soko la vitenge na kanga nyingi kutoka nje huku viwanda vya ndani vikikosa soko.

CTI pia inataka kutoa zuio la maombi ya EAC CET kiwango cha asilimia 10 na kutoza ushuru wa asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye uzi wa pamba chini ya kichwa cha 52.05,52.06 na 52.07 isipokuwa kichwa kidogo cha 5205.23.00.

Jambo lingine ambalo wanataka liangaliwe upya ni uanzishwaji ushuru wa mapato wa asilimia 10 kwa mapato yanayotokana na Kupunguza Uzalishaji Uliothibitishwa (VER).

Baadhi ya hatua ambazo CTI ilisema imefurahishwa nazo ni pamoja na viwango vya sifuri vya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa pamba inayozalishwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Nyingine ni marekebisho ya jedwali la ada za serikali za mitaa za mabango na kuhodhi ili kupunguza viwango kutoka Sh. 10,000 hadi Sh. 7,000 kwa kila futi za mraba zisizo na mwanga na kutoka Sh. 13,000 hadi Sh. 10,000 kwa futi za mraba kwa mabango yenye mwanga.

**MJADALA BUNGENI**

Wakati CTI wakieleza mtazamo wao huo, bungeni jijini Dodoma jana wabunge waliendelea na mjadala wa mapendekezo ya bajeti hiyo, wakishauri serikali isizuie wafanyabiashara kuuza chakula nje ya nchi.

Mbunge wa Kalambo (CCM), Josephat Kandege, aliitaka serikali isiwazuie wafanyabiashara kuuza mazao nje ya nchi kwa kuwa uamuzi wake umesababisha kushuka kwa bei ya bidhaa hizo nchini.

Alisema kuwa kabla ya taarifa hiyo, mkulima alikuwa anauza gunia la mahindi kwa Sh. 70,000, lakini sasa limefika Sh. 40,000 hadi 30,000. Aliitaja ni hali inayowakatisha tamaa kuendelea na shughuli hiyo.

Mbunge wa Maswa Magharibi (CCM), Mashimba Ndaki, aliishauri serikali kuanzisha mfuko wa kuwasaidia wakulima pale bei za mazao zinaposhuka na kuweka ruzuku katika mbolea na pembejeo, ili kuwapa motisha wa kuendelea na shughuli hiyo.

Mbunge wa Viti Maalum, Kunti Majala, alimtaka Waziri wa Fedha kupandisha kodi ya mafuta ya kula yanayoingizwa nchini kutoka ya asilimia 25 hadi 50, ili wawekezaji wachukue malighafi zinazozalishwa ndani ya nchi na kuwapa motisha wakulima.

"Leo Waziri wa Kilimo anahamasisha watu kulima alizeti halafu Waziri wa Fedha anakwenda kuondoa tozo kwenye kilimo mnatuchanganya, zungumzeni, njooni na kauli moja ili tuokoe taifa letu kwenye suala la uzalishaji," alisema.

Ni hoja iliyomwinua Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akisema serikali haijapandisha wala kushusha kodi ya mafuta yanayoingizwa kutoka nje.

"Ninataka nitoe taarifa sio kwamba tumeshusha, tumebakiza ya mwaka jana kwa ajili ya kukabiliana na gharama za maisha, kwa maana hiyo wabunge wamesema hapa tupandishe sisi tumechukua hilo," alisema.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema serikali haijazuia wananchi kuuza bidhaa nje ya nchi isipokuwa wakulima wanatakiwa kufuata utaratibu wa serikali.

"Anayefuata utaratibu wa serikali kwa kupata kibali cha kusafirisha nje ya nchi, leseni ya biashara na TIN, kinyume cha hapo hatutoruhusu mazao ya kilimo kutoka nje ya nchi kinyume cha utaratibu," alisema Bashe.

Mbunge wa Segerea (CCM), Bonnah Kamoli, alimwomba Waziri wa Fedha kutoa fedha za ujenzi barabara mapema, ili kuharakisha utekelezaji wake kwa kuwa mara nyingi fedha zinatengwa, lakini utekelezaji unachelewa.

Mbunge wa Manyoni Mashariki (CCM), Dk. Pius Chaya, aliitaka serikali kuboresha mfumo kukusanya mapato unaojulikana kama Local Government Revenue Collection Information System kwa kuwa umekuwa na changamoto nyingi ikiwamo kutoa kumbukumbu namba ya malipo tofauti na iliyoandikwa.

***Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR) na Jenifer Gilla (DODOMA)**

# Mpina ambana Mwigulu matumizi ya trilioni 2.7/-

**Na Jenifer Gilla**

MBUNGE wa Kisesa, Luhaga Mpina, amemtaka Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuwasilisha bungeni jedwali linaloonyesha matumizi ya Sh. trilioni 2.75 za mikopo iliyochukua serikali kwa mwaka huu wa fedha.

Fedha hizo ni za mikopo ya Extended Credit Facility (ECF) na Uboreshaji wa Usalama wa Milki ya Ardhi (LTP) ambazo Mpina aliliambia Bunge jana kuwa zilipaswa kutumika kwa miradi ya maendeleo lakini zimetumika kwa mambo yasiyo na tija.

Mpina ambaye kitaaluma ni mchumi, pia alimtaka Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu aeleze alipata wapi mamlaka ya kuidhinisha mikopo hiyo ambayo ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeonyesha fedha zake zilitumika kwa matumizi yasiyo na tija.

**TRAB NA TRAT**

Akichangia bungeni jana asubuhi hoja ya mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, Mpina pia alionyeshwa kushangazwa na kitendo cha serikali kushindwa kukusanya fedha zinazotokana na malimbikizo ya kikodi Sh. trilioni 7.35 hadi kufikia Aprili 2023, ilhali kesi zipo katika mahakama za rufani za kodi, yaani TRAB na TRAT.

"Sasa unajiuliza Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka mzima umeisha tumeshindwaje kukusanya fedha hizi za TRAB na TRAT? Hizi mamlaka zetu zina changamoto gani kiasi cha kushindwa kukusanya hizi fedha?" Mpina alihoji.

Alisema uwezo wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kushinda kesi katika mashauri hayo ni asilimia 81. Ni hali aliyoitaja katika kesi hizo zenye malimbikizo ya Sh.trilioni 7.35, wana uwezo wa kukusanya Sh. trilioni sita alizotegemea zikusanywe katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mbunge huyo aliyewahi kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi katika uongozi wa Rais John Magufuli, alisema serikali imeweka mkazo katika kuwawekea kodi nyingi wananchi ili kupata mapato ilihali kuna fedha nyingi imeacha katika mahakama za rufani za kodi.

Mpina pia alisema kuwa hadi kufikia Aprili 2023, nchi ilikuwa na miamala ya fedha haramu Sh. trilioni 280 huku hakuna mikakati yoyote iliyowekwa na serikali kushughulikia fedha hizo. Inajikosesha mapato.

Alisema katika kipindi hicho, miamala iliyochambuliwa na FIU ni 769 kati ya miamala 16,035, hali inayoonyesha kuwa kuna ukwepaji na utoroshwaji fedha nje ya nchi uliopitiliza, hivyo kuchangia kuikosesha serikali mapato.

Aliishauri serikali kuweka wanajeshi kutoka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) katika mipaka na bandari bubu zilizopo nchini, ili kudhibiti biashara za magendo na kukusanya fedha nyingi za kuiletea nchi maendeleo.

# BoT yasisitiza marufuku dola kutumika kulipia mahitaji

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema Shilingi ya Tanzania ndiyo fedha pekee inayoruhusiwa kutumika nchini.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, alisema hakuna mtu au kampuni yoyote inayoruhusiwa kuikataa kwa malipo halali na kufanya hivyo ni kuvunja sheria ya benki hiyo ya mwaka 2006.

"Serikali ilishatoa tamko kuhusu katazo la matumizi ya fedha za kigeni kwa wakazi wa Tanzania katika kulipia bidhaa na huduma nchini. Maagizo yaliyokwisha kutolewa hapo awali kuhusu matumizi ya fedha za kigeni yanapaswa kuendelea kuzingatiwa kwa kuhakikisha bei zote hapa nchini zinatangazwa kwa Shilingi ya Tanzania," alisema.

"Bei hizi zinajumuisha kodi za kupangisha ardhi, nyumba na ofisi, gharama za elimu, huduma za afya, vifaa tiba na vitendanishi, gharama za usafiri, lojistiki na bandari, vifaa vya kielektroniki na huduma za mitandao ya mawasiliano."

Alisema malipo yanayoweza kufanyika kwa fedha za kigeni zinawahusu watalii na wateja wasio wakazi wa Tanzania.

"Bei hizi zinajumuisha gharama za hoteli, usafiri, viwanja vya ndege na visa kwa wageni, usafirishaji kwenda nchi za nje kupitia Tanzania na gharama za mizigo bandarini. Walipaji wanaotumia fedha za kigeni watambuliwe kwa vitambulisho vyao kama pasi za kusafiria na nyaraka za usajili kwa kampuni," alisema.

Alitaka viwango vya kubadilisha fedha vitakavyotumika viwekwe wazi na visizidi vya soko.

# Kibano chaja wanaochelewa kulipa mafao ya wastaafu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SIKU moja baada ya Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, kutangaza namba yake ya simu kwa umma kwa ajili ya kupokea malalamiko ya wanachama na wastaafu wa mifuko ya pensheni, amepokea ujumbe kutoka kwa watu 28.

Katambi alitangaza juzi bungeni namba hiyo baada ya wabunge na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kuhoji suala la wastaafu kusotea mafao kutokana na waajiri kutowasilisha kwa wakati michango yao katika mifuko ya PSSSF (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma) na NSSF (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii).

Katambi alisema jijini hapa jana kuwa serikali imetoa maelekezo tisa kwa mifuko hiyo na waajiri, ikiwamo kuhakikisha ndani ya siku saba kila meneja wa mkoa anawasilisha majina ya waajiri sugu wanaodaiwa michango ya wafanyakazi wao ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao.

Katambi aliwaambia waandishi wa habari jijini kuwa hadi jana, alikuwa amepokea ujumbe wa simu kutoka kwa watu 28. Kati yao, wanane wanailalamikia NSSF na 20 wana malalamiko dhidi ya PSSSF na tayari malalamiko saba yamefanyiwa kazi na kutatuliwa.

Alisema mifuko ina jukumu la kuhakikisha michango ya wanachama inawasilishwa na mwajiri kwa wakati.

"Ninafahamu pamekuwapo changamoto kwa baadhi ya waajiri kutowasilisha michango au kuwasilisha michango pungufu ya watumishi wao na kusababisha usumbufu kwa wastaafu na wanachama.

"Ninaelekeza wakurugenzi wakuu wa PSSSF na NSSF kuhakikisha mameneja wote wa mikoa wanasilikiza na kutoa elimu kuhusu taarifa za wanachama, yaani michango na mafao," alisema.

Pia aliagiza mameneja hao kuondoa malalamiko ya wanachama katika mikoa wanayoongoza na ndicho kitakuwa kipimo cha utendaji kazi wao. Pia waajiri wote walipe na kuwasilisha madeni ya michango ya watumishi wao kila mwezi.

"Baada ya Rais kupata meseji za wastaafu kumlalamikia au Makamu wa Rais au Waziri Mkuu au yeyote kupata malalamiko, tafsiri yake mteja huyo hajahudumiwa ipasavyo. Wapo ambao unabaini huyu mwananchi kwa meseji yake hii kama angekutana na ofisa wa PSSSF au NSSF angepata huduma bila usumbufu wowote.

"Kila mfuko uhakikishe mwanachama analipwa mafao ndani ya siku 60 za kisheria kwa wanachama ambao nyaraka zao zimewasilishwa kikamilifu kwenye mfuko na watumishi wa mifuko watapandishwa vyeo kwa kuzingatia utendaji na uwajibikaji katika kuwahudumia wateja," aliagiza.

Kuhusu waajiri, Katambi aliwataka kuwasilisha taarifa za kustaafu mtumishi miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu ili kuondoa ucheleweshaji wa mafao.

"Kutowasilisha michango ya wafanyakazi katika mifuko ni kosa kisheria, michango iwasilishwe katika mifuko bila shuruti na waajiri wasiotoa mikataba kwa wafanyakazi wao ni kinyume cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya mkutano wa Bunge la Bajeti kuhitimishwa, yeye na waziri wa ofisi hiyo, Prof. Joyce Ndalichako, watazunguka mikoa yote na watakapobaini kuna udhaifu hatua zitachukuliwa.

"Kuna waajiri hawawasilishi michango kwa kisingizio cha kujuana na kiongozi fulani wa serikali, sasa kujuana au urafiki na kiongozi haikusababishi wewe kuvunja sheria," alisema.

# Serikali yatoa msimamo wakimbizi toka Burundi

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

MKURUGENZI wa Idara ya huduma kwa wakimbizi nchini, Suddy Mwakibasi, amesema serikali haitatoa uraia kwa wakimbizi wanaoomba hifadhi kutoka nchini Burundi na kuwahamasisha waridhie kurejea nchini kwao.

Akizungumza kwenye Siku ya Wakimbizi Duniani ambayo kitaifa imefanyika kambi ya Nyarugusu wilayani Kasulu, amesema nchi ya Burundi kwa sasa ina amani na wanapaswa kurudi nchini humo kama suluhisho la kudumu.

"Nawasihi mwondoe ndoto ya kupewa uraia kwa kuwa kuna amani Burundi, nasikitika kuona kwanini mnaendelea kuishi kama wakimbizi badala ya kurejea nchini mwenu na kuendelea kujenga amani," alisema Mwakibasi. "Kigezo mnachotumia cha kupewa uraia kwasababu ya kuishi muda mrefu nchini hakipo kwenye sheria ya nchi kwa kuwa kukaa muda mrefu hakuondoi hadhi ya ukimbizi na nchi ndiyo inayotoa kibali cha uraia hivyo nawasihi mjiandikishe mrudi nyumbani," alifafanua Mwakibasi.

Alisema ikiwa wanataka kuwa raia wa Tanzania itawapaswa kwanza kurejea nchini kwao na kujivua hadhi ya ukimbizi na kisha kuomba uraia wakiwa raia huru kwa kufuata kanuni na taratibu za nchi.

Mwakibasi alisisitiza kuwa mwezi Novemba, mwaka huu, Serikali ya Tanzania na Burundi zitakutana katika kikao cha pamoja kutafuta namna bora ya kuwarejesha wakimbizi watakaokuwa bado wako kambini kwa kuwa kilichokuwa kinawafanya kukimbia nchini humo hakipo tena.

"Tulikaa kikao mwezi wa tano mwaka huu na kuweka mikakati ya urejeaji wa wakimbizi itakayoanza kupimwa mwezi wa sita, ikifika mwezi Novemba, tutakaa tena kuona namna nyingine yakufanya."

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Mwenyekiti wa Wakimbizi Kambi ya Nyarugusu, Asende Meshak, kuomba serikali na Shirika linalohudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) kutoa suluhisho la kudumu kwa wakimbizi kwa kuwapatia uraia au kuwawezesha kwenda kuishi nchi ya tatu.

Alisema hiyo ni kutokana na changamoto za uraia usioleweka kwa wakimbizi wengi kutokana na wengi wao kuzaliwa na kukuliaTanzania jambo linaloleta mkanganyiko katika kutambua uraia wa mtu husika.

Ndikubwayo Kiza, raia kutoka nchini Burundi alisema yupo kambini Nyarugusu kwa miaka 36 na kwamba hayupo tayari kurudi nchini kwao kwa kuwa hajui namna ya kuanza maisha.

Charles Robart kutoka Congo DR alisema ni ngumu kurejea nchini kwao kutokana na vurugu za chinichini ambazo zinasababisha kukosa amani, kushindwa kufanya maamuzi ya kurudi nyumbani au wengine kuamua kwenda kuwa wakimbizi nchini Uganda.

Hata hivyo, Ndikumana Bhikulayo mkimbizi kutoka Burundi aliiomba serikali kuwasikiliza ili kubaini wenye matatizo wapewe uraia na ambao hawana warundi nchini mwao, kwa kuwa sio wote wanaogoma kurudi nyumbani hawana sababu za msingi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

eGA

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu**

**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

# Majaliwa: Serikali haitodharau maoni, ushauri suala Bandari

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewahakikishia Watanzania serikali haitodharau maoni na ushauri wanaoutoa kuhusu maeneo yenye hofu kwenye mradi wa uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Pia amewataka Watanzania kuendelea kuwa na imani na serikali na wawakilishi wao ndani ya Bunge, kwa kuwa imejizatiti kuhakikisha bandari inakuwa na ufanisi unaoendana na mahitaji ya sasa na kwa kuzingatia manufaa ya kijiografia ya nchi.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 40 ya Chuo cha International Evangelism Centre kilichoko Sakila jijini Arusha.

Alisisitiza bandari haijauzwa, bali serikali inataka kubadilisha mwekezaji ili iendeshwe kwa ufanisi na tija zaidi.

Alisema pamoja na maboresho yaliyofanyika, hali ya utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam imeendelea kuwa ya kiwango cha chini kulinganishwa na bandari shindani kikanda.

"Kwa mfano, wastani wa meli kusubiri nanga kwa Bandari ya Dar es Salaam ni siku tano kulinganishwa na wastani siku moja na nusu kwa Bandari za Mombasa na Durban," alifafanua.

Alisema udhaifu huo uliopo katika bandari hiyo unasababisha meli kusubiri muda mrefu nangani na hivyo kuongeza gharama, kwa siku moja ni takriban Dola za Marekani 25,000 kwa siku.

Waziri Mkuu alisema kitendo cha meli kutumia muda mrefu kupakia na kupakua shehena gatini kwa wastani wa siku tano, kulinganishwa na siku moja inayokubalika kimataifa, kinasababisha meli kubwa kutokuja katika Bandari ya Dar es Salaam.

Majaliwa alisema hali hiyo huikosesha nchi mapato ambayo yangeweza kutumika katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati nchini ambayo ingesaidia kukuza uchumi na kuboresha huduma za wananchi.

Waziri Mkuu alisema ili kutatua changamoto za bandari zilizopo na kuongeza ufanisi katika mapato, ajira na kuchagiza sekta nyingine za kiuchumi, serikali ilifanya uamuzi wa kutafuta wawekezaji wapya wanaoendana na dhima yake.

Majaliwa alisema Juni 10, 2023, Bunge liliridhia mkataba unaohusu makubaliano ya uhusiano baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai (IGA), ili kuwezesha majadiliano ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Alisema miradi hiyo ni pamoja na ya uendelezaji na uboreshaji wa huduma za bandari nchini.

"Kilichofanyika sasa ni kuwezesha tu baadaye kuwa na mikataba ya maeneo maalum ambayo itazingatia maslahi ya nchi kisheria na kibiashara bila kuathiri usalama Taifa," alisema.

Majaliwa pia alisema wakati wa kuingia mikataba utakapofika, wataalamu wa uchumi nchini wataishauri serikali kuhusu muda wa uendeshaji wa uwekezaji huo, hivyo akawataka wananchi waendelee kuwa na subira.



Meneja wa Mradi wa Amani Yetu, Mshikamano Wetu unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya, Maria Kiombo, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hafla ya ufungaji wa mradi huo itakayofanyika Juni 27, mwaka huu, mradi huo umesaidia kuimarisha masuala ya kidemokrasia. Kulia ni mratibu wa mradi huo, Almas Mohammed. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sheria Makosa ya Mtandao kupitiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali (DTP) inaendelea kupitia sera, sheria na mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusu TEHAMA ikiwamo Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Kundo Mathew, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira.

Mbunge huyo alihoji mpango wa kuhuisha Sheria ya Makosa ya Mtandao na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi pamoja na Mkataba wa Malabo.

Akijibu swali hilo, Kundo alisema serikali imekamilisha utungwaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyotiwa saini Novemba mwaka jana na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Desemba 2, mwaka jana na sheria hiyo imeanza kutumika rasmi Mei Mosi mwaka huu.

Naibu Waziri huyo alisema kuwa hayo yanafanyika kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi zaidi ya utekelezaji wa masuala mbalimbali yanayohusiana na TEHAMA, nchini ikiwamo kufanikisha kufikia azma ya uchumi wa kidijitali.

"Serikali kupitia mradi wa DTP inaendelea na mapitio ya sera, sheria na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa inayohusu TEHAMA. Sheria zinazofanyiwa mapitio kwa ajili ya kuhuishwa ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015," alisema.

Vilevile, alisema mikataba ambayo utaratibu umeanza kwa ajili ya kuridhiwa ni pamoja na Mkataba wa Malabo.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema kwa kuwa mkataba wa Malabo unaweka msingi wa makosa ya mtandao, ulinzi wa taarifa binafsi pamoja na biashara mtandao.

"Kwa kutambua fursa zinazotokana na soko huru la Afrika la biashara mtandao lini serikali italeta azimio hapa bungeni la kuridhia mkataba huu wa Malabo ili Tanzania isiendelee kuchelewa kupata fursa hizo?" alihoji.

Pia alihoji lini Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imeanza kutumika na hatua za serikali kutunga kanuni ili kulinda taarifa hizo na kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia mtandaoni.

Akijibu maswali hayo, Kundo alisema Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, Mei 6, mwaka huu alitia saini Kanuni za Sheria ya Ulinzi wa Taarifa na zipo tayari kwa ajili ya kutumika.

Kuhusu azimio, Naibu Waziri alisema serikali iko katika mchakato wa kupeleka azimio la Mkataba wa Malabo bungeni. Sheria ya Makosa ya Mtandao ni miongoni mwa sheria zinazolalamikiwa na wadau wa haki za binadamu kwa madai ya kuminya uhuru wa habari nchini.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janeth Mahawanga, alihoji lini Kanuni za Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016 zitahuishwa na wadau kushirikishwa ipasavyo.

Akijibu swali hilo, Kundo alisema wiki iliyopita Bunge lilipitisha marekebisho ya sheria hiyo na inatarajiwa baada ya Rais kutia saini, waziri atatangaza siku ya kuanza kutumika na mchakato wa kanuni zitakazoendana na mabadiliko hayo utashirikisha wadau.

## Serikali yashauriwa kupitia upya masharti ya WB, IMF

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imeshauriwa kupitia upya sera na masharti ya mikopo inayopokea kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia (WB), ili kuimarisha sekta ya umma, huduma za jamii na maslahi ya watumishi.

Pia, imeshauriwa kuweka mikakati ya kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma kila mwaka bila kujali masharti kutoka IMF na WB ili kuwapa motisha, kukuza ufanisi na kuwawezesha watumishi wa umma kukidhi mahitaji yao.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na kikundi kazi cha haki kodi cha Policy Forum, wakati wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya utafiti kuhusu sera za WB, IMF na hali ya watumishi kwenye sekta ya umma katika nchi 15 duniani ikiwamo Tanzania.

Akizungumza katika mkutano huo, Ruth Mlemba, alisema miaka 40 iliyopita Tanzania ilijiunga na mpango wa mabadiliko ya kiuchumi uliolenga kupunguza gharama na ukubwa wa sekta ya umma, kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kukuza sekta binafsi.

Alisema mpango huo uliratibiwa na WB pamoja na IMF, kutokana na sera hizo za kubana matumizi sekta ya umma Tanzania imeathirika zaidi na kupunguzwa kwa wafanyakazi wengi.

"Sekta ya umma haikuajiri wafanyakazi wapya na wale waliobaki ndani ya ajira walibaki na mishahara midogo isiyokidhi mahitaji. Sera hizo za kubana matumizi zimeleta matokeo hasi hususani kwenye utoaji wa huduma za jamii zikiwamo afya na elimu," alisema Mlemba.

Alisema utafiti walioufanya umeonyesha kwamba sekta ya elimu na afya kwenye nchi nyingi duniani ndizo zilizoajiri watu wengi kati ya theluthi moja hadi nusu ya wafanyakazi wote, wengi wakiwa ni wanawake.

Hivyo, alisema serikali inapaswa kuongeza idadi ya wafanyakazi wa umma ili kukabiliana na madhara yatokanayo na ugonjwa wa virusi vya corona, mabadiliko ya tabianchi.

Alisema pia WB, IMF zinapaswa kufanya tathmini ya sera zao kuona ufanisi wake, namna ya kuepusha madhara yaliyotokea kwa zaidi ya miaka 40 iliyopita.

Alisema serikali, IMF na WB zinapaswa kuongeza uwazi ili kujua masharti yaliyopo katika kukopa pia kuwapo kwa mazungumzo ya mzigo mkubwa wa madeni kwa nchi maskini kama Tanzania.

"Ikiwezekana madeni yaweze kufutwa au kuongeza muda wa kulipa. Hii itasaidia kuboresha utoaji wa huduma za jamii."

Naye Israel Ilunde kutoka muunganiko wa kikundi hicho alisema sera za WB, IMF zimekuwa zikiathiri watumishi wengi wa umma hasa kwenye sekta ya elimu na afya.

Alisema sera hizo zimeleta athari ikiwamo ongezeko la mshahara kwa sekta ya umeme imekuwa ndogo kutoka Sh. trilioni 9.83 mwaka 2022/23 hadi Sh.trilioni 10.882 kwa mwaka 2023/24.

# Wakulima waeleza kero uingizwaji mafuta nchini

**Na Maulid Mmbaga,** aliyekuwa DODOMA

WAKULIMA wa alizeti nchini wamesema thamani ya zao hilo imeshuka kutokana na uingizwaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Ili kulinda ajira na ustawi wao, wakulima hao wameiomba serikali kudhibiti uagizaji wa mafuta nje ya nchi.

Omari Issa, mkazi wa Chamwino, aliiambia Nipashe juzi kuwa msimu uliopita walikuwa wanauza alizeti kwa bei inayoendana na gharama walizotumia wakati wa kulima, lakini msimu huu imeshuka baada ya mafuta mengi kutoka nje kuingia nchini.

Issa ni Mwenyekiti wa Kikundi cha Izaku kinachojihusisha na kilimo cha alizeti. Alisema kuwa awali kulikuwa na uhaba wa mafuta ya kula nchini na serikali ikaruhusu kuingizwa mafuta ya nje na madhara yake imewaletea shida kwa bei ya alizeti.

Alishauri utaratibu huo usitishwe kwa manufaa ya wakulima wa ndani kwa kuwa kwa sasa uzalishaji wa alizeti umeongezeka.

"Awali uhaba wa mafuta ulikuwa unatokana na kwamba tulikuwa tunapanda mbegu za kienyeji, lakini kwa sasa kupitia ufadhili wa Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT) kwa kushirikiana na Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI), Rubi na Tafamo wametuletea mbegu bora za alizeti ikiwamo Super fine ambayo imetuongezea mavuno kwa kiasi kikubwa.

"Mwanzo tulikuwa tunapata magunia matatu kwa ekari moja lakini sasa baada ya kuanza kutumia mbegu bora, tunavuna magunia 10 kwa ekari moja.

"Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha mafuta mengi kupita hata Ukraine, hivyo tunaiomba serikali na wadau wa kilimo kuendelea kutuletea mbegu bora," alitamba Issa.

Aliongeza kuwa kupitia mradi wa AMDT wa kuhamasisha matumizi ya mbegu bora ya alizeti, kwa sasa mavuno yameongezeka kwa kiasi kikubwa na wamefanikiwa kupata zaidi ya kilo milioni 12 kwa msimu huu.

Alieleza kuwa baada ya kupata mavuno kwa wingi, malengo yao ni kutengeneza mnyororo wa thamani wa zao hilo, ikiwamo kuweka miundombinu ya maghala na mashine zitakazowawezesha kukamua mafuta kwa wingi na kuongeza ajira kwa vijana.

Makamu Mwenyekiti wa Kikundi cha Izaku, Happiness Sadala, alisema kupitia mradi wa AMDT, vijana wengi wamepata ajira huku wengine wakilima mashamba yao wenyewe baada ya kuwezesha mbegu bora na vifaa vya kisasa vya kulimia.

"Pia kwa wanawake imetusaidia kwa sababu awali tulikuwa hatuna vikundi, lakini baada ya kuanza huu mradi tumeunda vikundi mbalimbali na kupitia hivyo tumepatiwa elimu na kutumia mbegu bora na vifaa vya kisasa na kuacha kutumia jembe la mkono, imesaidia sana kuongeza kiwango cha mavuno katika msimu huu.

"Awali ugumu ulikuwa unapanda eneo kubwa lakini unapata mazao machache kutokana na vifaa na mbegu iliyokuwa inatumika, lakini kwa sasa unapanda ekari chache unapata mazao mengi kwa kuwa tumepatiwa vifaa vya kisasa na mbegu bora," alisema Happiness.

Serikali imekuja na mikakati mbalimbali kuhakikisha kunakuwa na uzalishaji mkubwa wa mafuta ya kula nchini. Takriban Sh. bilioni 400 hutumika kila mwaka kuagiza mafuta ya kupikia nje ya nchi.




Mkuu wa Mauzo Airtel Zanzibar, Mussa Sultan na Balozi wa Airtel, Lukas Muhavile maarufu (Joti), wakigawa zawadi ya pikipiki mpya kwa mshindi wa kwanza Nickson Molel kwenye hafla maalum iliyofanyika Zanzibar. Upige Mwingi ni promosheni ya miezi mitatu ambayo inatoa fursa kwa mtumiaji yeyote wa huduma za Airtel kujishindia zawadi kama muda wa maongezi, pikipiki, TV, friji na fedha taslimu kuanzia Shilingi milioni moja kwa siku mpaka milioni 50. Kulia ni Meneja Mauzo, Nassoe Twahil. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

# 'Mshtakiwa alibadilisha nguo kabla gwaride la utambulisho'

**Na Grace Gurisha**

MKAGUZI wa Polisi, Henry Kambalire, amedai mahakamani kuwa mfanyabiashara Revocatus Muyela (40), anayetuhumiwa kumuua mdogo wa marehemu Erasto Msuya, Aneth Msuya, alibadilisha nguo kabla ya kufanyiwa gwaride la utambulisho.

Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni aliyekuwa mke wa bilionea huyo, Miriam Mrita. Inadaiwa kuwa Aneth aliuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Imedaiwa mahakamani kuwa shahidi ambaye alikuwa ni dada wa kazi wa marehemu Aneth, Getruda Mfuru, aliweza kumtambua mshtakiwa huyo licha ya kwamba alibadili nguo kabla ya utambuzi.

Mkaguzi huyo alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wake, akieleza jinsi alivyoandaa gwaride la utambulisho na mshtakiwa Muyela katika Kituo cha Polisi Kilwa Road.

Alidai kuwa Agosti 21, 2016, alikuwa katika kituo chake cha kazi, ambapo kwa wakati huo alikuwa na cheo cha Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, alipata maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa (RCO), Mchovu, kuwa aendae gwaride la utambulisho.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Generosa Montano, Kambalire alidai alimwamuru Sajenti Emmanuel amlete mshtakiwa eneo la gwaride ambapo alijitambulisha kwake na yeye alijitambulisha kwake kuwa ni Revocatus Ernest.

Alidai kuwa alimweleza haki zake za msingi mshtakiwa kuhusu gwaride la utambulisho kuwa ana haki ya kwenda kusimama sehemu yoyote kwa washiriki wanane, aliowaandaa kwa ajili ya utambuzi kulingana na mwonekano na maumbile yao.

Pia alidai alimweleza kuwa ana haki ya kubadilisha nguo kutoka kwa washiriki hao na haki yake nyingine ni kwamba anaweza kumwita ndugu au wakili kushuhudia gwaride hilo.

"Mshtakiwa aliamua kubadilisha mavazi (shati) kutoka kwa washiriki hao na alipomaliza alimweleza kwamba 'hakuna shida wanaweza kuendelea' na alisimama nafasi ya pili kutoka mwisho.

Baada ya hapo, Zakati alimleta shahidi Getruda Mfuru katika gwaride, alizunguka mbele na nyuma kwenye mstari na kisha kumgusa mshtakiwa Muyela kwenye bega na kudai kuwa huyo ndiyo mhusika.

Alidai mshtakiwa alirudishwa mahabusu na yeye alijaza fomu ya polisi namba 186 kuhusiana na gwaride hilo, ambapo kabla ya Mfuru kufanya zoezi hilo Kambalire alimweleza majukumu yake ya kufanya.

Akijibu maswali ya Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, shahidi huyo alidai kuwa kazi yake ilikuwa ni kusimamia gwaride sio kujua historia za watu kama mshtakiwa alikuwa hana ndugu wala wakili Dar es Salaam.

Pia alidai aliyekuwa na jukumu la kuingiza majina katika fomu ya polisi namba 186 ni msimamizi wa kesi hiyo na siyo yeye na pia gwaride hilo la Agosti 21, 2016 ndiyo ilikuwa la kwanza kwake kulifanya.

Katika maelezo ya onyo, Miriam anadaiwa aliamua kumuua wifi yake kwa sababu alikuwa anamfuatafuata katika suala la usimamizi wa mirathi ya mumewe, Bilionea Msuya na katika kutekeleza mauaji hayo alimkodi mtu ambaye alimlipa Sh. milioni 20.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 21/06/2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatano** tarehe **21/06/2023** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM**, gari hilo lenye namba za usajili:

Gari hizo zenye namba za usajili:
**T 175 DFN / T 168 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18.00, Upana - mita 2.80, Kimo - mita 5.00**

3. Njia itakayotumika: **SINGIDA** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **MOROGORO**. Gari itasafiri muda wa mchana tu (**kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**



CLINTON FOUNDATION | CLINTON DEVELOPMENT INITIATIVE
TREES for the FUTURE

## INVITATION FOR SUPPLY OF FOREST GARDEN ITEMS

The Clinton Development Initiative (CDI), an initiative of the Clinton Foundation in partnership with the Forest Trees For The Future (TFTF) are implementing Forest Garden project in Iringa and Kilolo Districts. The project aims at providing families with sustainable food sources, livestock feed, products to sell, fuel wood and up to a 400% increase in their annual income. The CDI in Iringa under the auspices of the TFTF now invites interested suppliers to apply for the supplying and delivery of Forest Garden Items as presented in the table below:

| Item No. | Item Description | Qnty | Unit |
|---|---|---|---|
| 1 | Biodegradable trees sacs | 6992 | Packs |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

The invitation to supply the said items shall be valid for a period of seven days from the date of appearing in the newspaper. Interested supplier must submit a letter of application giving quotes for the items in full. Late applications shall be rejected. Applications will be opened at the below address on June 27th, 2023 10:00am in the presence of the suppliers who wish to attend. CDI reserves the right to accept or reject any applications, and to cancel the procurement process and reject all applications at any time prior to award of Contract, without obligation to inform the affected supplier/s of the ground for CDI action.

**Send sealed application letter with quotation to:**
**Country Agribusiness Manager**
**Clinton Development Initiative | Clinton Foundation**
**Hailey Selassie Street**
**Gangilonga Area**
**P.O Box 792 Iringa**
**Tanzania**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jiulize umeitumiaje mvua msimu huu?

**MWEZI** Juni unaelekea ukingoni na kuashiria kuanza msimu wa kuvuna mazao na kuwapa Watanzania punguzo la bei ya vyakula sokoni lakini pia fedha mifukoni kwa wakulima popote walipo.

Ni matumaini yetu kuwa baadhi ya mazao ya chakula kama mtama, mihogo, ngano, viazi, magimbi, mpunga, mahindi na ya biashara kama pamba, alizeti, ufuta yatavunwa vya kutosha na bei za vyakula kuwa na ahuweni sokoni.

Wakati msimu wa masika unaondoka na kukaribisha majira ya kipupwe, tungeshauri kila mmoja kujitazama, amenufaikaje na mvua za msimu huu?

Ni kwa sababu inasikitisha kuwa bado watu hawapendi kujihusisha na kilimo hata kama mvua zipo za kutosha.

Mathalani, kwenye majiji mfano Dar es Salaam, licha ya mvua kubwa kunyesha tena kwa miezi karibu mitatu wengi hawana hata mche wa mboga kama maboga, matembele na bamia au matunda hasa papai na matango.

Si kwamba ardhi yote mijini ina wakazi, kuna sehemu kuna viwanja lakini havijajengwa, yapo mapori na mashamba ambayo wamiliki hawajayaendeleza ni vyema kuyatumia kulima.

Tunakumbusha kuwa wakati mwingine kunapokuwa na neema ya mvua kama mwaka huu viongozi wa kiserikali wilayani na mikoani wawahamasishe wananchi mijini kulima kwa kukumbuka kuwa kilimo kina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa taifa na familia.

Kumbukeni kilimo ndicho kinachoajiri asilimia 65.5 ya watu na huchangia asilimia 29.1 ya pato la taifa, 30 ya mazao yanayouzwa soko la nje na asilimia 65 ya malighafi za viwandani, hivyo kuna haja ya kuongeza hamasa hasa mijini ili watu walime.

Vijana jijini Dar es Salaam pengine wana mitizamo kuwa kilimo huenda ni cha watu maskini, wanaona ni bora kuendesha bodaboda au kuuza pweza na ngisi pembeni ya barabara ili kupata fedha haraka kuliko kuingia shambani kulima mihogo, mbaazi, ufuta, papai na viazi.

Ni vyema kukiwa na majira ya mvua kama ilivyotokea msimu huu wanasiasa wakawahamasisha watu kulima hasa wakazi wa mijini, ni kwa sababu walio wengi hawajihusishi na kilimo kwa sababu wana fikira kuwa ni kazi ya wanaoishi vijijini.

Hata hivyo, licha ya kuona kuna mvua ya kutosha zile fikra kuwa kilimo ni cha watu wa rika fulani kama wazee au wanawake zinatawala na kufifisha ari ya vijana wengi kulima, hivyo kwa pamoja tuhimizane kulima na kuzalisha chakula chetu wenyewe.

Ni wakati wa kuachana na fikra potofu ambazo zinashuhudia mvua zikimalizika na kuacha watu wengi mikono mitupu. Kilimo si cha watu waliofeli darasani, wengi wanaichukulia hii dhana kana kwamba kilimo ni kwa jili ya walioshindwa maisha si hivyo.

Maisha yanazidi kuwa magumu iwapo watu hawatajishughulisha na uzalishaji mathalani wa mazao kama mihogo, viazi na mbaazi hasa wakazi wa ukanda wa pwani ambao wengi mko mijini.

Leo hii bei ya mahindi ya kuchoma jijini Dar es Salaam iko juu kama kijana ungelima mahindi ni wazi ungeinuka kiuchumi kwa kuuza moja 500 na kama yapo mashina 2,000 unaweza kupata hata Shilingi 800,000 baada ya kutoa gharama.

Kilimo cha mapapai nacho kingekuinua mkazi wa mjini iwapo ungepanda msimu mvua ilipoanza kwani yangekuwa yanaanza kuchanua na kutoa maua kisha matunda.

Kwa hiyo msimu wa mvua unapomalizika utukumbushe kuwa tusirudie makosa tunapoona mvua zinanyesha kama ilivyotokea mwaka huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Ingefaa mgombea huru akubalike

Na Sabato Kasika

**SUALA** la nchi kuwa na mfumo unaoruhusu mgombea binafsi, ni la muda mrefu ambalo hadi sasa halijapatiwa ufumbuzi, huku ikielezwa kuwa kuwapo kwa mgombea huyo kunaweza kupanua demokrasia.

Baadhi ya wadau wa siasa wanafafanua kuwa Ibara ya 21(1) ya Kàtiba ya Tanzania, inaruhusu kila Mtanzania kushiriki shughuli mbalimbali ikiwamo kuwania uongozi katika vyama vya siasa au kuchaguliwa.

Mfumo unaotumika katika kupata uongozi wa kisiasa, ni lazima kupitia chama, utaratibu ambao wanaeleza kuwa unawafanya baadhi ya Watanzania wasio kwenye vyama kukosa nafasi hizo.

Binafsi ninaunga mkono mtazamo huo, kwani kupitia katika vyama hakuwezi kupanua wigo wa demokrasia, kwani baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakilalamika kubaniwa na viongozi wa vyama vyao.

Kwa mfano, mtu anaweza kujitokeza kuwania uongozi, lakini kama kiongozi wa chama hamtaki, hawezi kuteuliwa au kuchaguliwa, hivyo ni wazi kwamba suala la kuwapo mfumo wa mgombea binafsi linafaa.

Hivyo, ninadhani ni vyema iwapo Watanzania wakawa huru wa kushiriki katika siasa bila kupitia vyama, kwani mfumo huo unaweza kurudisha nyuma harakati za kila Mtanzania kushiriki shughuli za maendeleo.

Mgombea binafsi ni sakata lililoibuliwa na aliyekuwa mwenyekiti wa Chama cha DP, Mchungaji Christopher Mtikila (marehemu), zaidi ya miaka 20 iliyopita, ingawa sasa halina nguvu kama enzi ya uhai wake.

Kimsingi, suala la mgombea binafsi, ni mjadala wa muda mrefu tangu ambao uliibuliwa na mwanasiasa huyo pale alipofungua kesi ya kikatiba katika Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma.

Kesi hiyo ilisikilizwa na Jaji Kahwa Lugakingira, ambaye alikubaliana na hoja zake na kusema kugombea kama mtu binafsi ni haki ya kila raia kwa mujibu wa katiba na kufafanua kuwa aliye na haki ya kuchagua viongozi ana haki pia ya kugombea uongozi.

Lakini baadaye serikali iliwasilisha bungeni mapendekezo ya kubadilisha Ibara ya 34 ya Katiba kwa kuzuia wagombea binafsi.

Lakini mwaka 2005, Mtikila alifungua tena kesi nyingine katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam akipinga marekebisho hayo.

Baada ya kufungua kesi hiyo, lilikaa jopo la majaji watatu waliokuwa wakiongozwa na Jaji Amir Manento, ambao nao kwa pamoja walikubaliana na hoja za mwanasiasa huyo, lakini baadaye serikali ikakata rufani kupinga hukumu hiyo.

Hoja ya serikali katika Mahakama ya Rufani, ilikuwa ni kwamba hakuna mahakama yenye uwezo wa kusikiliza shauri la mgombea binafsi kwa maelezo kuwa inaingilia kazi za kibunge.

Aidha, pamoja na Mahakama ya Rufani kukubali haki ya kila raia kuchagua na kuchaguliwa bila kuwa mwanachama wa chama cha siasa, ilisema si jukumu la mahakama kujielekeza katika mambo ya kisiasa.

Baada ya hukumu hiyo, safari ya milima na mabonde ya mgombea binafsi ikaanza, kwani Mchungaji Mtikila alifungua kesi namba 011 katika Mahakama ya Afrika na Haki za Binadamu, mwaka 2011.

Mwaka 2013, hukumu ya kesi hiyo ilitolewa akawa ameshinda, huku serikali ikitakiwa kuchukua kuijulisha mahakama kuhusu utekelezaji wa hukumu hiyo iliyompa ushindi Mchungaji Mtikila.

Lakini serikali ikaeleza kuwa mfumo wa mgombea binafsi ungeangaliwa katika katiba mpya, kwa kuwa mchakato wa katiba hiyo ulikuwa ukiendelea. Hata hivyo, mwanasiasa huyo alifariki dunia mwaka 2015 huku suala mgombea binafsi likiwa halijapatiwa ufumbuzi hadi leo.

Tangu wakati huo, ni kama hakuna mwanasiasa aliyebeba mikoba ya Mchungaji Mtikila ya kuendeleza harakati za kutaka serikali kuruhusu mfumo wa mgombea binafsi.

Nguvu kubwa za wanasiasa ni kama zimeelekezwa katika kudai tume huru ya uchaguzi na katiba mpya.

Yote hayo ni muhimu, lakini hata suala la mgombea binafsi lingepewa uzito, ili kuondokana na mfumo wa sasa.

Kuwapo kwa mfumo, kunaweza kusaidia kuondoa ukiritimba wa kubaniana kati ya viongozi wa vyama na wanachama, ambao unatajwa kushamiri kwenye baadhi ya vyama hivyo.

HABARI KITAIFA

# Chongolo apokewa kwa mabango ya kero

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amepokewa na mabango yenye kuelezea kero ya zahanati na shule ya sekondari, akiwa kwenye ziara yake Kata ya Dalai, wilayani Chemba mkoani hapa wakati msafara wake ukiwa njiani kwenye Kijiji cha Chandama.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wenzake wa Kijiji cha Dalai jana, Diwani wa Kata ya Dalai, Shabani Mateleka alisema, kijiji hicho hakina zahanati na wananchi wanalazimika kutembea zaidi ya kilometa 20 kufuata huduma za afya Kata ya Mrijo.

"Wajawazito wanapata shida wakati wa kujifungua na kulazimika kutumia gharama kubwa kutafuta usafiri kwenda hospitali," alisisitiza.

Mateleka alisema wananchi walianza kujitolea juhudi zao na ujenzi upo kwenye msingi na nguvu hiyo imeshia hapo na kuiomba serikali kuwasaidia ujenzi huo.

Kero nyingine alitaja ni shule ya sekondari kuwa mbali na kuwalazimu wanafunzi kutembea kilomita zaidi ya saba kwenda Shule ya Sekondari Mondo.

Alisema walianza ujenzi kwa nguvu ya wananchi na wameahidiwa kusaidiwa ujenzi huo, lakini hawaoni juhudi hizo kukamilika.

Mbunge wa Jimbo la Chemba, Mohamedi Moni, alisema eneo hilo pia linakabiliwa na tatizo la kituo cha afya na hulazimika kufuata huduma hiyo Mrijo kilomita zaidi ya 20.

Moni alisema, eneo hilo kuna kata zaidi ya sita na hakuna kituo na kuomba huduma hiyo kwenye makao makuu ya kata eneo la Mondo.

Pia alisema halmashauri ya wilaya hiyo inakabiliwa na tatizo la maji kwenye baadhi ya vijiji hasa kipindi cha kiangazi inawachulia muda mwingi kutafuata huduma hiyo.

Chongolo aliwashukuru wananchi hao kwa kuwasilisha kero zao.

"Mlichofanya ni sahihi mimi nipo hapa kwenye ziara ya kukagua na kusikiliza kero za wananchi na tupo wilayani kilio chenu nimekisikia wananchi," alisema.

Katibu Mkuu huyo wa CCM, aliwachangia mifuko ya saruji 50 na fedha tasilimu Shilingi milioni moja kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Dalai.

Kuhusu shule ya sekondari alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, kushughulika hilo pamoja na uongozi wa Halmashauri ya Chemba kukamilisha mapema ili wanafunzi waanze masomo.

Akiwa kwenye ziara hiyo, Chongolo aliwahamasisha wazazi kuwajengea maadili mema watoto wao ili kuondoa vijana wanaovaa ovyo mitaani.

"Nashukuru nimeona vijana wa hapa wamevaa kistaha inaonekana mmewafundisha vizuri, lakini siku hizi kuna vijana wanavaa vibaya njiani hivyo naomba msiache kuwajengea maadili vijana watoto wenu,"alisihi.

# Taasisi 300 serikali zatumia gesi kulinda mazingira

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI za serikali 369 zimeunga mkono agizo la kuacha kutumia kuni na mkaa na kuingia katika matumizi ya nishati safi na salama (gesi).

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, iliagiza taasisi zote za serikali kuacha matumizi ya mkaa na kuni ili kuokoa mazingira yanayoharibiwa.

Akizungumza kwenye mafunzo ya waandishi wa habari wa Mkoa wa Morogoro kuhusu kampeni ya utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi na salama, Meneja wa mauzo kwa wateja wa Taifa Gas Tanzania Limited, Moses Massawe, alisema lengo lake ni kukomesha uvunaji wa miti kiholela.

Massawe alisema, Taifa Gas inaunga mkono juhudi za serikali katika suala la uhifadhi na utunzaji wa mazingira na kuweka mkakati wa utoaji wa elimu ya madhara ya matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema kutokana na elimu inayotolewa na kuendelea kutolewa, taasisi 369 za umma zimeunganishwa na nishati safi na salama.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hizo, Taifa Gas kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka huu imeweka mkakati kuzifikia taasisi 460 na kuwa jumla ya taasisi 829.

Mkuu wa Chuo cha Ualimu Morogoro, Augustine Sahili, ambaye chuo chake kimeachana na matumizi ya kuni na mkaa baada ya kuunganishiwa gesi, alisema tangu kuanza kutumia nishati hiyo wameokoa Sh. milioni 15 kwa mwaka.

"Kwa sasa tunapika chakula kwa muda mfupi na nafuu kuliko mkaa na kuni kwa mwezi ni Sh. milioni 4.5 hadi milioni 4.8 na sasa tunatumia Shilingi milioni tatu kwa matumizi ya gesi na kuokoa Sh. milioni 15 kwa mwaka," alisema Sahili.

Meneja wa Corporate Affairs wa Taifa Gas, Angela Bhoke, alisema taifa linaendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, wana wajibu kusaidiana na serikali kudhibiti ukataji miti kwa ajili ya kuboresha mazingira.

Bhoke alisema, Mkoa wa Morogoro umetajwa kuwa miongoni mwa mikoa iliyoathirika zaidi kwa ukataji miti na ni mkoa wenye mito mingi ambayo ni vyanzo vya maji yanayotegemewa kwa wananchi wa mikoa mingine ya Pwani na Dar es Salaam.

Pia alisema, kampeni ya utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati salama kwa mazingira safi katika awamu ya kwanza inahusisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga na Tabora.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

## TANGAZO KWA UMMA

### KUANZA KWA UNUNUZI WA AKIBA YA CHAKULA YA TAIFA KWA MSIMU WA 2023/2024

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha akiba ya chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula na majanga mengine ya Kitaifa yanayoweza kujitokeza.

**NFRA** hununua nafaka kila mwaka kwa ajili ya akiba ya chakula ya Taifa. Kwa mzimu huu wa mavuno ununuzi utaanza rasmi tarehe tarehe 22 Juni, 2023.

**Mazao na Malengo ya Ununuzi:**

- Mahindi tani 200,000
- Mpunga tani 200,000

**Njia za Ununuzi Zitakazotumika:**

- Kutumia vituo vya ununuzi-Muuzaji yeyote anaweza kupeleka nafaka zake kuuza;
- Vikundi vya Wakulima/Ushirika-Vitaingia makubaliano maalum na NFRA;
- Mawakala/wafanyabiashara wa mazao - Wataingia makubaliano maalum na NFRA.

**Vituo vya Ununuzi:**

Kwa kuanzia, NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa mahindi kwenye kanda zifuatazo zenye uzalishaji na upatikanaji mkubwa wa nafaka; Songea (Mkoa ya Ruvuma), Makambako (Mikoa wa Njombe na Iringa), Songwe (Mikoa wa Songwe na Mbeya), Sumbawanga (Mikoa ya Rukwa na Katavi), Dodoma (Dodoma na Manyoni), Arusha (Arusha na Manyara) na Shinyanga (Mkoa wa Kigoma na Tabora). Aidha, mpunga utanunuliwa katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Songwe, Mbeya na Tabora.

**Utaratibu wa Ununuzi:**

Nafaka zote zitakazofikishwa katika vituo vya NFRA, zitapokelewa iwapo zitakidhi vigezo vya ubora kama vitakavyobainishwa kupitia Kanda za NFRA. Bei elekezi zitakazotumika zitapangwa kwa kuzingatia umbali kutoka ghala kuu la NFRA na bei za soko katika eneo husika. Utaratibu wa ununuzi wa nafaka kupitia Vyama vya Ushirika/Vikundi vya Wakulima na Mawakala utafanyika kupitia makubaliano yatakayofikiwa baina ya Kanda ya NFRA na Vyama/Vikundi husika.

# TIB yaadhimisha utumishi kwa usafi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo TIB, imeanza kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2023 kwa kufanya usafi kwenye Kituo cha Daladala Simu 2000, Ubungo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa zoezi hilo lililofanyika mwishoni mwa wiki, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TIB, Lilian Mbassy, alisema benki imeamua kushiriki kufanya usafi katika eneo hilo ili kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya serikali kipindi hiki cha Wiki ya Utumishi wa Umma inayoadhimishwa kuanzia Juni 16 hadi 23, kila mwaka.

"Tukiwa sehemu ya watumishi wa umma tunaunga mkono juhudi za serikali katika masuala ya usafi na mazingira hasa katika wiki hii ya utumishi wa umma nchini," alisema.

Aliongeza kuwa TIB itaendelea kuwa mdau wa maendeleo wa Manispaa ya Ubungo kwa kuwa Balozi wa Usafi wa Manispaa hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Voster Mgina, alipongeza benki hiyo kwa kujitoa kwao kwenye masuala ya usafi na alitumia nafasi hiyo kuwakaribisha kushiriki shughuli nyingine za kijamii katika Manispaa ya Ubungo.

TIB walikabidhi vifaa mbalimbali vya kufanyia usafi vitakavyosaidia shughuli za kuiweka Manispaa ya Ubungo katika hali ya usafi.

Vifaa vilivyokabidhiwa ni matoroli (2), mifagio (80), vikusanya usafi (20) na ndoo za kuhifadhi uchafu (12), vifaa vyengine ni pamoja na reki (20), glovu (200) na viatu vya kufanyia usafi (30).




Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Kampala, kilichopo Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam, Anna Sombe (katikati), akitwanga kwenye mafunzo ya kutengeneza mkaa mbadala kwa kutumia maboksi ambayo yanafanyika katika Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake kuhamasishwa udereva taxi mtandao

**Na Romana Mallya**

MENEJA Mkazi wa Kampuni ya usafiri kwa njia ya Taxi-Mtandao (Bolt) upande wa Tanzania, Charles Matondane, amesema kampuni yao inahakikisha suala la usawa wa kijinsia ndani ya nchi linafikiwa kwa kuhamasisha wanawake wengi kujiunga na kutoa huduma hiyo.

Matondane aliyasema hayo baada ya kuteuliwa na kampuni hiyo kushika wadhifa huo mpya upande wa Tanzania.

Alisema Bolt inathamini madereva wake wote na inatambua kuwa wana jukumu muhimu katika ukuaji endelevu wa kampuni na kuhakikisha wanafikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote kujingiza kwenye biashara hiyo ili kujiongezea kipato.

"Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) yaliyopitishwa na Umoja wa Mataifa (UN) hasa lengo la tano linalotaka kuwapo na usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake ni nguzo kuu ya kazi.

"Tunaamini kwamba tuna fursa ya kuchangia katika kuziba pengo la kijinsia kwa kuruhusu wanawake kujiajiri katika nafasi ya kidijitali ya kutuma taxi mtandao," alisema.

Pia alisema wanajitahidi kuwahimiza na kuhakikisha kuwa madereva wanawake, wasafirishaji vifurushi, pamoja na abiria wanafurahia huduma.

Kuhusu usalama wa watumiaji alisema hicho ni kipaumbele chao kwa kuwa kampuni hiyo imetekeleza vipengele vya usalama vinavyoendelea kutathminiwa na kuboreshwa.

"Madereva wote kwenye kampuni hii hupitia mchakato mkali wa uthibitishaji na wanatakiwa kuwasilisha hati husika kabla ya kujiunga. Madereva ambao hawazingatii sheria na masharti ya ushiriki wamezuiwa kutumia mfumo wetu," alisema.

Alisema wana mfumo wa kutoa alama kwa dereva na mteja ambao huruhusu madereva na waendeshaji kukadiria kila baada ya safari.

"Tunachukua ukadiriaji huu kwa umakini sana na kuzuia madereva na watumiaji ambao wana alama za chini sana kutumia mfumo wetu. Tunawatia moyo madereva wafanye kazi kwa heshima wakati wote wanapokuwa kwenye mfumo wetu," alisema.

Matondane mwenye Shahada ya Kwanza katika Biashara na IT pamoja na Diploma ya Uzamili katika Sayansi ya Data na Uchanganuzi wa Biashara, alisema lengo la kampuni yao ni kutegemea ukuaji katika soko na kutoa fursa za kiuchumi kwa wote.

"Kwa kushirikiana na kampuni vijana wakitanzania wanaweza kuongeza uwezo wao wa kuongeza mapato kupitia utaratibu wa kufanya kazi ambao unanufaisha pande zote mbili," alisema.

Alisema kampuni hiyo inatoa fursa ya wazi ya kujiajiri kwa watu wa rika zote kujiunga na biashara na kutumia ubunifu wao na fikra kujiongezea kipato.

## Kampuni kuboresha sekta huduma vyakula nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuboresha huduma za vyakula vya hotelini nchini, kampuni ya Foodex imetangaza mkakati mpya wa kuchangia jitihada za serikali za kukuza uchumi na maendeleo ya taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Foodex, Safa Erzurumlugil, alisema kampuni yake kwa kuona Tanzania imeboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji, ni muda mwafaka kushiriki katika juhudi za kuiunga mkono Serikali ya Tanzania.

"Tumedhamiria kufanya mapinduzi katika utoaji wa huduma za chakula na hoteli Tanzania na kuzifanya zikidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa na pia kwa lengo la kuvutia wageni, watalii na wawekezaji katika sekta mbalimbali za uchumi. Lengo ni kutoa huduma bora za vyakula zinazowavutia wageni wengi, wanaokuja kufanya biashara na kutalii hapa kwetu," alisema Erzurumlugil.

"Tumejizatiti kuisaidia serikali kutimiza ndoto zake kwa kufanya mapinduzi na maboresho makubwa katika huduma za chakula na hoteli... kutoa huduma zenye viwango na bora kwa wageni, watalii na wawekezaji kutoka sehemu mbalimbali duniani kuja kutembelea na kuwekeza nchini Tanzania."

Alisema huduma nzuri ya vyakula zinazokubalika kitaifa na kimataifa ni jambo lisiloepukika.

"Ukuaji wa biashara na uwekezaji utahitaji utoaji wa huduma bora za chakula na zingine zinazoendana na mahitaji ya soko. Ndiyo maana Foodex imekuja na mkakati mpya ambao utahakikisha Watanzania na wageni wanaofanya biashara nchini wanapata huduma bora na tuko hapa kwa kazi hiyo."

Alisema huduma zitakazotolewa na kampuni hiyo zitatumiwa na aina zote za matukio ya kijamii, kitaifa, kikanda na kimataifa na kwamba wateja (watu binafsi, taasisi za serikali, mashirika ya kitaifa na kimataifa) watapata uzoefu wa aina yake (wa vyakula) kwa sababu kampuni hiyo imejipanga kutoa huduma tofauti na zenye ubora.

Kadhalika, alisema huduma walizonazo ni pamoja na zinazoendana na upishi wa kimataifa wa nchi za Italia, India, China na milo mbalimbali inayolenga mahitaji ya wateja.

"Foodex imekuja na mikakati itakayoiwezesha kushindana kikamilifu kwa kutoa huduma nzuri za chakula na hoteli Tanzania, huku ikizingatia sera, sheria, kanuni, usalama wa afya na kuweka mazingira katika hali ya usafi."



## Waziri afichua siri vituo vya afya huduma mbovu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amesema usimamizi hafifu wa vituo vya afya nchini husababisha vituo hivyo kutoa huduma zisizoridhisha.

Amesema pia kutotumia fedha kwa wakati zinazotokana na mapato ya uchangiaji wa huduma za afya, mfuko wa afya wa pamoja na Global Fund inachangia vituo kuwa na bakaa kubwa.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati akifungua kikao kazi cha siku mbili cha waganga wakuu na waratibu wa UKIMWI wa halmashauri nchini, kilichoenda sambamba na uzinduzi wa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa za mfumo wa mshitiri.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari 2023 kupitia Mfuko wa Global Fund, Sh. bilioni 32.2 zilitumwa katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali, ikiwamo uboreshaji wa miundombinu.

Pia alisema hadi kufikia Januari, 2023 Sh. bilioni 4.9 bado hazijatumika, kwamba hali hiyo inasababisha nchi kukosa fedha zingine za ujenzi wa miundombinu husika.

Vile vile, alitumia fursa hiyo kuwaagiza wakurugenzi wa halmashauri, waganga wakuu wa mikoa na halmashauri nchini, waganga wafawidhi wa vituo kuongeza uwajibikaji wa kusimamia vituo hivyo ipasavyo na kuhakikisha fedha zote zilizopo vituoni, zinatumika kwa wakati na kuzingatia mipango.

Alisema Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kusimamia huduma za ustawi wa jamii katika eneo la familia, malezi, makuzi, maendeleo ya awali ya mtoto, huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu.

Alisema hadi kufikia Februari mwaka 2023 watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 335,971 walitambuliwa kati yao 26,000 sawa na asilimia 7.7 walipewa huduma mbalimbali kama chakula, malazi, mavazi na matibabu.

Vilevile, alisema mashauri 13,926 ya ukatili wa kijinsia yaliripotiwa, kati ya hayo 7,142 sawa na asilimia 56 yalikuwa ni mashauri dhidi ya wanawake na 6,784 sawa na asilimia 51 yalikuwa ukatili dhidi ya watoto, ambapo mashauri 1,199 yalifikishwa mahakamani kati ya hayo 430 sawa na asilimia 36 yalitolewa hukumu.

"Naendelea kuwasisitiza waganga wakuu wa halmashauri moja kuhuisha kamati za ulinzi kwa wanawake na watoto, katika ngazi zote mbili, kuhakikisha mashauri ya kesi za watoto, ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, unasimamiwa ipasavyo mahakamani, huku wakiendelea kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuwaunganisha na huduma stahiki," alisema.

Pia alisema uzito pungufu umepungua kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia 12 mwaka 2022 na ukondefu umepungua kutoka asilimia tano mwaka 2015, hadi asilimia tatu mwaka 2022.

Kadhalika alisema, jukumu kubwa la TAMISEMI ni kuendelea kusimamia afua za lishe, ikiwa ni pamoja na kupeleka huduma za lishe katika ngazi ya wananchi.

Alisema ili kufikia dhima hiyo ni lazima viongozi ngazi ya mikoa na halmashauri kuhakikisha wanatekeleza haraka zaidi afua za lishe katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

Hivyo aliagiza halmashauri ziendelee kutenga Sh.1,000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano, katika maeneo yao na kuhakikisha kuwa usimamizi unafanyika, ili zitumike kutekeleza afua za lishe zenye kuleta matokeo chanya na ya haraka.

# Wabunge EALA wajitosa sakata uwekezaji bandari

**Na Allan Isack,** ARUSHA

BAADHI ya wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) kutoka Tanzania, wametoa hadhari kwa wanasiasa wanaozungumzia vibaya uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam, kwa muktadha wa ubaguzi, udini na eneo analotokea kiongozi husika.

Kundi hilo la wabunge, limeeleza wasiwasi wake kama hatua zisipochukuliwa mapema hali hiyo inaweza kuleta madhara kwenye suala la muungano.

Wakizungumza jana jijini Arusha, baadhi ya wabunge akiwamo Dk. Makame Abdullah Hasnuu, alisema baada ya Bunge la Tanzania kupitisha azimio kuhusu pendekezo la kuridhiwa kwa mkataba baina ya Serikali ya Tanzania na Dubai, kumezuka mijadala yenye lengo la udini na ubaguzi inayoendeshwa na baadhi ya wanasiasa.

Dk. Makame, alisema viongozi wa dini, kisiasa na wananchi, wanapaswa kuimarisha umoja, amani, upendo, utawala bora na kukemea kila aina ya ubaguzi.

"Tunakemee jambo hilo na tunapaswa kurejea katika umoja wetu, tuheshimu katiba yetu, sheria na tukemee aina zote za ubaguzi ya kumbagua Mtanzania kutokana na dini, kabila na ukanda wake," alisisitiza.

Aidha, mbunge mwingine, Machano Ali Machano, alisema kiuhalisia Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na kila mtu ana haki ya kutoa maoni au mawazo yake kwenye jambo husika, ila kuna baadhi ya watu wanatumia vibaya uhuru huo.

"Kuna maeneo yanazungumzwa mitaani na kwenye mitandao ya kijamii, yenye sura ya ubaguzi wa kikanda na udini. Jambo hili halina afya kwetu," alieleza Machano.

Wakati Nadra Juma Mohammed, alisema kutokana na tamko hilo tayari wamemwomba Msajili wa Vyama vya Siasa, kuangalia sheria na kuwachukulia hatua kali, hasa viongozi wa kisiasa wanaokwenda kinyume na utaratibu.

Juni 10, mwaka huu, Bunge la Tanzania, lilipitisha azimio kuhusu pendekezo la kuridhiwa kwa mkataba wa DP World, baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai, kwa lengo la kuanzisha ushirikiano katika uendelezaji wa maeneo ya bandari nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kushoto), akikaribishwa na Mkurugenzi wa Mji wa Mbulu, Yefred Myenzi, kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2021/2022, halmashauri hiyo ilipata hati safi jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Watoto waiomba serikali kuwadhibiti wanyamapori

**Na Cynthia Mwilolezi,** LONGIDO

TISHIO la wanyamapori kuvamia makazi ya watu katika Wilaya ya Longido, mkoani Manyara, limewasukuma watoto wilayani humo kuiomba serikali kuwadhibiti ili kunusuru maisha yao.

Waliwasilisha ombi hilo kwa serikali jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika kiwilaya katika Kata ya Tingatinga. Kauli mbiu ya mwaka huu ni 'zingatia usalama wa mtoto katika ulimwengu wa kidijitali.'

Kwa nyakati tofauti, Paskalina Ismail, mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Longido na Ngaangaa Mseeni, ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Ngereiyani, walisema wamekuwa wakikutana na wanyama wakali, wakati wa kwenda shule kama tembo, chui na duma, hali ambayo inahatarisha usalama wao.

Kutokana na tishio hilo wameiomba serikali kuimarisha ulinzi maeneo yote ya elimu ili wasivamiwe na wanyama na kujeruhiwa au kuuawa.

Vilevile, Paskalkna alisema watoto wa wilaya hiyo wapo kwenye mazingira magumu, kwa kuwa licha ya kuzungukwa na wanyama wakali pia baadhi yao wanashinikizwa na wazazi kutokwenda shule ili waolewe na kuchunga mifugo.

"Hali hii inasababisha baadhi yetu kukatisha masomo na kukimbilia nchi jirani ya Kenya, ambako wanafanya shughuli za uchimbaji wa madini.


Aidha, wamelishukuru shirika lisilo la kiserikali la Casee, kwa kuwasaidia kupata elimu, huku wakiwahimiza wadau wengine kujitokeza kusaidia wanafunzi wanaotokea jamii ya kifugaji ya Kimasai kupata elimu.

Ofisa Elimu, Ulinzi na Usalama wa Mtoto wa Shirika la Casee Child Fund Korea, Wivini Mtende, akizungumza na jamii ya wakazi wa Tingatinga, alisema mradi huo umekuwa ukihudumia shule nne za msingi za Kata ya Tingatinga na Namanga.

Shule zinazonufaika na mradi huo ni Buguruni, Tingatinga, Namanga na Ngareiyani, ambako kumejengwa shule tano shikizi ili wanafunzi wa jamii ya Kimasai waweze kusoma karibu na maeneo wanayotokea.

Diwani wa Tingatinga, Peter Lekaneti, alisema miradi ya elimu inayosimamiwa na shirika hilo, imetoa mwangaza mkubwa katika kata yake, huku likimaliza pia tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Atuganile Chisunga, alisema hadi kufikia sasa wameokoa wavulana 21 ambao walikuwa wakienda nchi jirani ya Kenya, kwa ajili ya kufanya kazi za kuchunga mifugo pamoja na ulinzi.



# Wanafunzi walioacha masomo kwa ujauzito warejeshwa

**Na Timothy Itembe,** MARA

WANAFUNZI 26 wilayani Tarime walioachishwa masomo baada ya kupata ujauzito wamerejea shuleni, kuendelea na masomo huku wengine nane wameokolewa kutoka nchini Kenya walipokuwa wakitumikishwa kwenye ajira, ombaomba.

Akizungumza na Nipashe juzi, Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Antoni Nyange, alisema kuwa katika halmashauri hiyo imefanikiwa kuwarudisha shuleni wanafunzi hao na sasa wanaendelea na masomo ili kutimiza ndoto zao za kielimu.

"Wengine nane wenye ulemavu wa viungo wameokolewa kutoka nchi jirani ya Kenya walipokuwa wamepelekwa kinyamera kutumikishwa na kufanya biashara ya ombaomba na wamerudishwa makwao Bariadi," alieleza.

Aidha, alitoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanawalinda watoto wao dhidi ya ukatili wa kijinsia unaowazunguka na ambao umekithiri kwa sasa unaosababisha wanafunzi hao kushindwa kupata haki zao za kimsingi.

Alisema watoto hao wenye ulemavu walipatikana nchini Kenya kwa ushirikiano baina yao na maofisa wa Serikali ya Kenya na kuongeza kuwa wazazi na walezi wanapaswa kusimamia maendeleo ya watoto wao wanapokuwa shuleni.

Naye Ofisa Miradi kutoka Shirika la AICT Dayosisi ya Mara na Ukerewe, Rebeca Zakayo, alisema kuna haja jamii kujua maendeleo yanayotokana na ulimwengu wa kidijitali na kuwafundisha watoto wao kuepuka athari zinazotokana na maendeleo ya vifaa vya kidijitali. Rebeka aliongeza kuwa wana mradi wa kuwafunza watoto kujua kusoma na kuandika kwa lengo la kukuza ubora wa elimu jumuishi, kwamba wanatoa vifaa saidizi kwa watoto wenye ulemavu wa viungo mbalimbali katika miili yao.

Aidha, Diwani Kata ya Itiryo, Shadrack Marwa alisema kuna haja jamii kuachana na mila zilizopitwa na wakati badala yake itumie muda huo kusomesha watoto bila kujali jinsia zao ili kuwatimizia haki zao za kimsingi.

Alisema: "Pia jamii iondoe dhana hasi kwa watoto wenye ulemavu kwani sasa hivi tunao viongozi wengi wenye ulemavu na hili ni zao la kuwasomesha, bila elimu hawezi akawa kwenye nafasi yoyote lazima tuwajali kwa maslahi yao na taifa kwa ujumla."




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Latifa Khamis (katikati), akishika mkasi kwa ajili ya kuzindua rasmi tuzo za Consumer Choice Awards Africa (CCAA) jana jijini Dar es Salaam. Kulia ni Diana Laizer ambaye ni mwanzilishi wa tuzo hizo na wengine ni wadhamini wa tuzo hizo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# M-Mama yazinduliwa kudhibiti vifo vya mama, mtoto

**Na Titus Mwombeki,** KAGERA

SERIKALI mkoani Kagera kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wamezindua rasmi mpango maalumu wa M-MAMA unaolenga kutoa huduma kwa ukaribu zaidi na mjamzito na watoto ili kupunguza vifo vya mama na mtoto mkoani humo.

Akizindua mpango huo mwishoni mwa wiki, Katibu Tawala Mkoa wa Kagera, Toba Nguvila, alimesema kuwa viongozi wa mkoa huo wanatakiwa kuunga mkono mpango huo ili kuweza kumweka salama mama na mtoto na kuokoa maisha yao.

"Maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha hakuna vifo vya mama na watoto wakati wa kujifungua ambavyo vimeweza kuzuirika hivyo hii ni huduma muhimu sana ya kuhakikisha mama anakuwa salama katika kipindi cha ujauzito na kuhakikisha anakuwa salama," Nguvila.

Aidha alieleza kuwa kwa sasa vifo vimepungua mkoani humo kutoka 55 kwa mwaka 2020 hadi vifo 42 kwa mwaka 2022 na kwa Januari mpaka Machi mwaka huu vimetokea vifo 13.

Aliwataka viongozi wa halmashauri wanatakiwa kutenga fungu la kutosha kuwasaidia kinamama wajawazito wanapoitaji msaada wa kwenda kujifungu huku akisisitiza kuwa wataingia mikataba na watu binafsi wenye magari yatakayotumia kama magari ya kusafirishia wagonjwa.

Mratibu wa mama na mtoto Mkoa wa Kagera, Neema Kyamba, alisema kuwa zimekuwapo sababu mbalimbali zinasababisha vifo kwa mama na mtoto ikiwa pamoja na uwezo mdogo kwa watoa huduma za uzazi kwa mama na mtoto, uzembe pamoja na uchache wa watumishi katika vituo vya afya suala linalosababisha kuelemewa na wateja.

# Machimbo ya dhahabu kugeuzwa kuwa eneo la uwekezaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga imesema eneo lililokuwa likitumiwa kwa ajili ya uchimbaji dhahabu la Buzwagi lililopo wilayani Kahama mkoani Shinyanga lililositishwa shughuli zake za uchimbaji litakuwa eneo la uwekezaji.

Imesema lengo likiwa ni kuhakikisha eneo hilo linaendelea kutumika. Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, wakati akizungumza na viongozi wa dini, wazee maarufu na machifu kutoka mkoani humo na kueleza kuwa kwa sasa serikali inatafuta mwekezaji atakayekuwa tayari kutumia eneo hilo.

Alisema serikali kuu imetoa Sh. bilioni 612.3 na kutekelezwa miradi mbalimbali ya maendeleo, lengo likuwa ni kuukuza Mkoa wa Shinyanga kiuchumi na kusogeza huduma mbalimbali na za muhimu kwa wananchi.

"Eneo hilo ni zaidi ya hekta 1,330 ambalo lilikuwa likitumiwa na mgodi wa Buzwagi kuchimba madini ya dhahabu eneo hilo tumeligeuza kuwa kitovu cha uchumi, litaitwa 'Samia Special Economic zone' na vitajengwa viwanda vingi kwa sasa tunakaribisha wawekezaji,"alisema Mndeme.

Aidha, alisema hivi karibuni akiwa na viongozi wengine wa Wilaya ya Kahama, walitembelea Falme za Kiarabu katika eneo la Dubai Textile City, ili kujifunza na kukaribisha wawekezaji waje kuwekeza katika eneo hilo la machimbo ya Buzwagi na pia atakutana na wafanyabiashara mkoani humo ili kuwahamasisha wachangamkie fursa hiyo.

Alisema pia serikali mkoani humo katika Wilaya ya Kahama, wametenga tena zaidi ya ekari 2,000 kwa ajili ya kujengwa bandari kavu ambayo itakuwa chanzo cha ukuaji wa uchumi mkoani Shinyanga pamoja na kukarabati viwanja vya ndege.

Katika hatua nyingine Mndeme, aliwataka viongozi wa dini, wazee maarufu na machifu mkoani humo, kumuunga mkono Rais Samia katika uwekezaji wa bandari ambao umelenga kukuza uchumi kwa wananchi na kupuuza maneno ya upotoshaji.

Nao wazee maarufu, viongozi wa dini, na machifu wakitoa tamko lilisomwa na Chifu Charles Njange Kidola, alisema hatua ya serikali kuendelea kutoa fedha za maendeleo mkoani humo sambamba na kutekeleza miradi mbalimbali itasaidia kuupaisha mkoa huo kimaendeleo.


Ukurasa 12

**Tanzania kufuta maelfu ya asasi kulivyoistua dunia**


Ukurasa 13

Uhalifu wa ADF Uganda unavyotishia usalama EAC



Ukurasa 14

**WAZIRI MWIGULU NCHEMBA Anatisha jimboni anabebwa juu juu asijikwae, wapigakura wakiri amefanya maajabu Iramba**


# siasa

JUMATANO JUNI 21, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


KATIBA KWA MASILAHI YA TAIFA

# Ulinzi muungano, rasilimali, maisha bora kufuta umaskini

**Na Dk. Felician Kilahama**

MASILAHI kwa taifa letu yanatakiwa yawe ni sehemu ya katiba ya Tanzania, ni suala nililolianza wiki iliyopita, hivyo huu ni mwendelezo wa makala hiyo.

Kimtazamo baadhi ya maeneo muhimu kitaifa au nguzo yanayobeba masilahi hayo ni pamoja na usalama kwa Watanzania wote, hivyo mkazo uwe ni kulinda usalama wa taifa na watu wake.

Kipaumbele ni uhai wa Watanzania ikiwamo walioko nje ya nchi ili kwamba ikitokea jambo fulani linalohatarisha usalama wao taifa lichukue hatua za haraka kuwahakikishia usalama.

Vilevile ihakikishe maliasili muhimu zinahifadhiwa kwa faida ya kizazi hiki na vitakavyofuata, dhamira kuu iwe ni kuwezesha watu kuishi kwa amani, utulivu na kujiletea maendeleo endelevu.


Katiba mpya imalize umaskini na maisha duni ya Watanzania. **PICHA: MTANDAO**

**MUUNGANO UDUMU**

Tanzania mipaka yake iwe imara na salama na ndani ya nchi kumetulia. Kwa usalama zaidi suala la kuimarisha Muungano linahitaji kutiliwa mkazo. Kwa wakati wote taifa liwe tayari kukabiliana na chochote ambacho kinaweza kuhatarisha usalama wa nchi na watu wake. Nia iwepo, uwezo uwepo na ari ya kutosha iwepo.

**KUTOKOMEZA UMASKINI**

Kuhakikisha wananchi wanakuwa na maisha bora mijini na vijijini ni suala la masilahi ya taifa: Maisha bora kwa kila Mtanzania ni suala muhimu sana ikiwa ni pamoja na uhakika wa chakula na makazi bora. Turejee kwenye misingi ya mwasisi wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, mathalani, Azimio la Arusha na kanuni zake, ikumbukwe ni muhimu na hayajapitwa na wakati yazingatiwe.

Kuutokomeza ufisadi, rushwa, dawa za kulevya na ubadhirifu wa fedha na mali za umma ni lazima, kuwapo siasa safi, uongozi bora na madhubuti pamoja na uwajibikaji imara kwa ngazi zote.

Tuwe wakweli na bila kudhulumu misingi muhimu ya uongozi turejee kwenye kanuni zilizokuwapo mfano, miiko ya uongozi na maadili mema katika utumishi wa umma. Kuwa na mali au tajiri si dhambi ila zipatikane kihalali na siyo kinyume cha hapo, huku haki ikitendeka kwa masilahi ya wote;

Kutunza, kusimamia, kulinda na kutumia vizuri maliasili pamoja na rasilimali nyingine za taifa, kama fedha na watu kwa masilahi ya wote.

Mfamo, ardhi ipo tena ya kutosha itumike na vyote vilivyo juu au chini yake kwa manufaa ya wote. Nguvu kazi hasa vijana, itumike ipasavyo kwa bidii na kwa akili na maarifa ili yote yanayofanyika yalete tija kwa mhusika na taifa.

Watanzania wote tuone maliasili tuliyonayo kuwa ni urithi wa kitaifa hivyo tuwajibike kuilinda na kuitumia kwa njia endelevu na kwa faida ya wengi;

kuboresha masilahi ya watumishi serikalini na katika sekta binafsi ni muhimu. Ikumbukwe mishahara na 'marupurupu' viendane na hali halisi ya maisha. Kupunguza tofauti kubwa iliyopo kati ya viongozi wa juu kwenye siasa, watendaji ngazi za juu serikalini na watumishi ngazi za kati na chini.

Watumishi wa ngazi za juu mishahara ni mikubwa na marupurpu pia manono, wakati ngazi za kati na chini mishahara haikidhi mahitaji ya kila siku na marupurupu kama yapo ni finyu.

Je, hali hiyo kwa mustakabali na masilahi ya taifa letu ni sahihi? Hivyo, sera na kanuni za utumishi wa umma pia kwa sekta binafsi, ziandaliwe kwa umakini mkubwa ili kuleta uwiano kimasilahi kwa ngazi zote za utumishi. Suala hili liangaliwe kwa kina ukizingatia kwamba wote tunajenga taifa letu kwa faida ya wote. Kusiwe na mwelekeo wa kuwepo matabaka ya makabila na makabwela haipendezi.

kuimarisha na kudumisha utamaduni na utu wa Mtanzania, kinachotakiwa, kwa mustakabali mzima wa taifa hili ni kuimarisha tamaduni zilizo na mielekeo mizuri kwenye dunia inayobadilika.

Wakati huo tukiheshimiana, wake kwa waume, tukithaminiana kwa uhalisia wetu wa rangi, kabila, imani, wageni tkuoka mataifa mbalimbali na wenye imani tofauti; kuwe na itikadi zinazodumisha utu, ubinadamu na siyo kinyume.

Taifa lisiendekeze udini bali watu wake wawe na uhuru wa kuabudu kulingana na imani zao, bila kuvunja sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kulingana na katiba itakayokubaliwa na wengi.

Tusiruhusu mienendo, yoyote ile, yenye nia ya kuvuruga na kutugawa Watanzania aidha kupitia masuala ya utamaduni, mathalani, kurejesha itikadi za kichifu na mambo yanayofanana na hayo au kutetea ukabila na masuala yanaendana na hayo ikiwemo kuchochea udini, kwa manufaa binafsi.

Haya ni miongoni mwa masuala ambayo madhara yake kwa taifa na watu wake ni makubwa, utu wa Mtanzania uambatane na hali ya kuheshimiana; wakubwa kwa wadogo; walionavyo na wasionavyo pamoja na watu wa itikadi tofauti kisiasa, kidini bila kujali rangi, elimu au wadhifa wa mhusika.

Kwa ujumla, tuwe na "miiko ya kitaifa" inayotambulika kikatiba maana taifa bila miiko inayoeleweka na kukubalika siyo jambo jema. Baba wa Taifa, aliwahi kutuasa kwamba taifa bila miiko mambo yake huwa 'ovyo ovyo'.

Hivyo, katiba inayotarajiwa iweze kuziba mapengo kama hayo kwa mustakabali, masilahi kwa taifa na wananchi wake. Makala hii iwe kichocheo kwa Watanzania kujadili suala la masilahi mapana ya nchi yao ili iwe sehemu ya katiba inayopendekezwa'. Kwa kuzingatia misingi na nguzo za taifa ndipo mipango mahususi ya muda mfupi na mrefu, pamoja na miradi ya kimkakati vitakapoandaliwa ili kukidhi mahitaji na malengo.

Pamoja na mipango itakayoidhinishwa, pia kuandaliwe ratiba za utekelezaji na bajeti husika kwa kila eneo kulingana na masilahi ya wengi. Vilevile, kuwapo na programu kabambe ya ufuatiliaji ili kuhakikisha wahusika

INAENDELEA UK. 12

# Tanzania kufuta maelfu ya asasi kulivyoistua dunia

•Vigogo Marekani, WB, UN-AIDS watua nchini kufanya ukaguzi

**Na Ani Jozeni**

UJIO wa hivi karibuni wa maofisa wa ngazi ya juu kutoka serikali ya Marekani, Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na UKIMWI (UNAIDS) haujatazamwa au kupewa kipaumbele katika vyombo vya habari, lakini inavyoelekea una lake jambo.

Inawezekana wapo walioelewa sababu halisi za ujio huo wakati wengine wangedhania ni wa kawaida, kwani Makamu wa Rais Kamala Harris alikuwapo nchini miezi kadhaa iliyopita.

Ukiangalia kwa 'jicho la tatu' unakuta yako masuala yaliyojificha, na kilichokuwa kinaendelea nchini wiki za kwanza za kuwasilisha makisio ya wizara kwa mwaka wa fedha ujao, unaweza kupata picha.

Sababu ni kuwa ujumbe huo ulilenga kuzungumza na vikundi vya kujitolea visivyo vya kiserikali Asasi za Kiraia (AZAKI) ambavyo zaidi vinashiriki mapambano na UKIMWI na penginepo kutoa ushauri kwa vijana, au kuwawezesha, wasipotee katika mustakabali wa kimaisha.

Ndiyo hapo unagusa mizozo ya kiitikadi kuwa mashirika yasiyo ya kiserikali yanatoa miongozo mibovu kwa vijana na taarifa za kuzuiwa usajili kwa takriban AZAKI (NGOs) 4,000 katika kipindi cha miezi sita iliyopita.

Ni hali ambayo inaweza kutilia shaka uhuru wa mashirika ya kijamii kufanya kazi nchini kwa uhuru unaoridhisha bila kuwa hatarini kufutwa wakati wowote.

Ndiyo hapo serikali ya Marekani, WB na UNAIDS wakaamua kuja wao wenyewe kuangalia na kuzungumza na wahusika, si kutumia tu taarifa za kibalozi au za ukaguzi wa ndani kuhusu misaada inavyotumika.

Yapo mambo katika uhusiano wa kimataifa yanayofanywa waziwazi na yako mengine yanayofanyika kimya, bila kutangazwa dhamira halisi.

Mojawapo ya njia za kugundua hali hiyo ni suala la wajumbe wanaofika nchini ambao ni zaidi ya kiwango kinachotazamiwa, kwa mfano misaada kwa mashirika ya kujitolea au yasiyo ya kiserikali, inasimamiwa na maofisa katika balozi au mashirika sambamba ya Umoja wa Mataifa nchini, huenda hayahitaji kukaguliwa na maofisa watendaji waandamizi kutoka wizara nchini Marekani kwa mfano.



Balozi Dk. Nkengasong
**PICHA: MTANDAO**

Wakipeleka ujumbe wa aina hiyo, kuna tatizo la ziada, kuwa wanataka tathmini ya kisiasa, haki za makundi yanayohusika zilivyo si kupima ufanisi.

Ndicho kilichoonekana hivi karibuni wakati taarifa za msisimko wa makundi yasiyo ya kiserikali kutokana na ujumbe wa mashirika ya wa fadhili hasa kuhusiana na mapambano dhidi ya UKIMWI duniani. Ujumbe mzito wa mashirika hayo ulileta tumaini kwa makundi ya hapa nchini kuweza kuonyesha wanachokifanya na labda wapate nafasi muhimu zaidi katika uwasilishaji wa huduma wanazotoa.

Deogratius Rutatwa, Ofisa Mtendaji Mkuu Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (NACOPHA) anawaambia wanahabari kuwa NGOs nchini zilikuwa na matazamio makubwa kwa ugeni mahsusi. Asingeweza kueleza nini cha ziada kimewaleta, kwani wasingeweza kuwa wakaguzi wa shughuli zao na usimamizi unaweza kufanywa na ubalozi au uwakilishi maalum. Ila watendaji wizarani wangekuwa na habari, wasiseme nini hasa kilihusishwa.

Kiashiria muhimu cha dhima ya ujio wa ujumbe huo ni kuwa ulizungumziwa na wenyeji wao, hasa NACOPHA na Wizara ya Afya hawakuita hafla yoyote juu ya ujio huo. Hiyo ni pamoja na kwamba aliyeuongoza ni Balozi Dk. John Nkengasong, mzaliwa wa Cameroon mwenye uraia wa Marekani ambaye ni Mkurugenzi wa Mtandao wa Vituo vya Kuzuia Magonjwa ya Mlipuko Barani Afrika vyenye uhusiano na Marekani (Africa CDCs), ambaye ni Mtawala Mkuu wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani kuhusu UKIMWI (PEPFAR), na hasa ni katika nafasi hiyo ambako alikuwa mgeni wa NACOPHA.

Ila kwa suala tu la ukaguzi wa shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI wasaidizi wake wangetosha kwa kazi kama hiyo. Isitoshe, kwa nafasi zake hizo, Balozi Dk. Nkengasong ndiye mratibu wa shughuli za Marekani kuhusu UKIMWI duniani kote, na mwakilishi maalum wa Marekani kwa masuala ya kidiplomasia kuhusu afya duniani.

Ndiyo maana kwa hali hiyo anakuwa ofisa mwandamizi zaidi katika serikali ya Marekani anayeweza kuongea na vikundi huria nchini vinavyotegemea misaada ya mashirika au nchi wahisani kwa shughuli tofauti kama UKIMWI, afya ya mama na mtoto, uhusishwaji wa vijana na haki za wote.

Walioshiriki wengine katika ugeni huo ni Peter Sands, Mkurugenzi Mtendaji wa Global Fund (mfuko wa kusaidia mapambano na UKIMWI ulio chini ya WB na Angeli Achrekar, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa UNAIDS.

Huenda suala lililowaleta inaelekea ni kufutwa kwa AZAKI zaidi ya 4,000 katika kipindi cha miezi sita, hali aliyokiri, Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) katika hotuba ya kuwasilisha makisio ya wizara hiyo.

Kufutwa kwa NGOs kwa maelfu kuliendana na mzozo wa kiitikadi kuhusu kuenea au kuenezwa kwa ushoga miongoni mwa vijana kuanzia watoto wa shule za msingi nchini, ambako kidole kilinyooshewa mitandao ya kijamii, baadhi ya vitabu na majarida ya mitaala tofauti shuleni na hasa shule binafsi.

Wanaofuatilia mahusiano kati ya serikali na AZAKI watakumbuka kuwa upo ushindani kati ya idara tofauti za serikali na vikundi huria au binafsi katika kupigania upatikanaji wa misaada ya kijamii katika eneo hili au lile.

(

# Ulinzi muungano, rasilimali, maisha bora kufuta umaskini

INATOKA UK. 11

wanawajibika ipasavyo ikiwamo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu pamoja na kudumisha maadili na miiko ya taifa.

Ni muhimu tukazingatia masuala haya kwa umakini ili kusiwapo na fursa za kupelekea au kuchochea wizi, rushwa, na udanganyifu kwa masilahi binafsi. Wawekezaji wakaribishwe lakini waelekezwe vizuri jinsi ya uwekezaji wao unavyoweza kuchangia uboreshaji wa maisha kwa kila mtanzania.

Kama ni kutengeneza bidhaa za kuuza nje ya nchi, matokeo yake, kwa kiasi kikubwa, yalete tija kwa nchi na kuboresha maisha ya Watanzania, kadhalika, tujifunze kutokana na makosa tusirudie makosa ili vizazi vitakavyofuata viweze kunufaika na rasilimali za kitaifa pamoja na kuwapo mazingira endelevu.

Yatakayokubalika na Watanzania walio wengi yawe ndiyo maeneo muhimu ya masilahi kwa nchi hii ikiwa ni pamoja na kudumisha haki, amani na furaha pamoja na kuwepo mshikamano wa kitaifa kwa faida ya wote.

# Uhalifu wa ADF Uganda unavyotishia usalama EAC



Mazishi ya baadhi ya wanafunzi wa Sekondari ya Lhubiriha waliouawa na ADF. **PICHA: AFP**

**Na Gaudensia Mngumi**

UGANDA imeshambuliwa na waasi wa ADF katika tukio linalotajwa na vyombo vya habari kuwa ni baya zaidi katika kipindi cha zaidi ya miaka 10 iliyopita, linaloua watu 41 wengi wao wakiwa wanafunzi mwishoni mwa wiki iliyopita.

Wanafunzi wa bweni la Sekondari ya Lhubiriha, iliyoko kilomita 2 kutoka mpakani na DRC lililochomwa moto Ijumaa usiku, na waasi hao wanaoua, kujeruhi na kuharibu miundombinu ya shule ni taarifa za vyombo mbalimbali vya habari duniani.

Mauaji hayo yanafanyika katika mji wa Mpondwe, karibu na mpaka na DRC, likifanywa na Allied Democratic Forces (ADF), kundi la waasi linalohusishwa na Dola la Kiislam la ISIL au ISIS ni taarifa za habari zilizoenea dunia kupitia media mbalimbali.

Wanafunzi walikuwa wamelala wakati watu wanaohusishwa na wapiganaji wa ADF walipowavamia, baadhi yao walikatwakatwa hadi kufa, huku wengine wakichomwa moto na kuunguzwa na mabomu ya petroli, hata wale walionusurika walijificha chini ya miili ya wenzao.

### NI KAMA MAZOEA

Ukiangalia mtiririko wa matukio unaona kuwa hili halikuwa shambulio la kwanza dhidi ya shule nchini Uganda kutoka ADF, Juni 1998, wanafunzi 80 walichomwa hadi kufa mabwenini katika shambulio la Taasisi ya Ufundi ya Kichwamba karibu na mpaka wa DRC. Aidha

> Waziri wa Elimu wa Uganda, Janet Museveni, mke wa Rais, anasema wanafunzi 17 wa kiume walichomwa katika bweni lao huku wanafunzi wa kike 20 wakikatwakatwa kwa mapanga hadi kufa baada ya ADF kuvamia Sekondari ya Lhubiriha.

zaidi ya wanafunzi 100 walitekwa nyara kwenye tukio hilo.

Halikadhalika, Uganda ilituhumu kundi hilo kwa mashambulizi mabaya ya kujitoa mhanga katika mji mkuu Kampala mwaka 2021, uhalifu uliotokea baada ya kuanzisha operesheni ya pamoja ya kijeshi nchini DRC.

Waziri wa Elimu wa Uganda, Janet Museveni, mke wa Rais, anasema wanafunzi 17 wa kiume walichomwa katika bweni lao huku wanafunzi wa kike 20 wakikatwakatwa kwa mapanga hadi kufa baada ya ADF kuvamia Sekondari ya Lhubiriha.

### SOMO KWA EAC

Kinachotokea Uganda sasa kutoka kwa ADF na pia Kenya ambayo ni mashambulizi yanayofanywa na kundi la al- Shabab kisipuuzwe, ni lazima nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zifanye kazi kwa pamoja kushughulikia uhalifu wa uasi, migogoro ya kivita na ukosefu wa usalama kwenye ukanda huo.

Wafanye kazi pamoja tena waongeze nguvu ya kwa misingi endelevu ikiwezekana kuwa na kamandi au kikosi maalumu cha kukabiliana na waasi hao.

Ni vyema Tanzania, Burundi, Rwanda, Uganda, DRC Sudan Kusini, kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema (early warnings) ya kubaini, kutumia mbinu za kukabiliana na mashambulizi ya kigaidi, kushughulikia na kudhibiti mashambulizi hayo kwani kinachotokea ndani ya nchi wanachama ni kama msemo wa ukiona mwenzio ananyolewa tia maji.

Hali ilivyo leo inataka kuwe na mifumo ya kukabili uasi kwa mbinu madhubuti kwa kuwa

> Ikumbukwe ukimbizi unaongeza hofu na kusambaa silaha hasa bunduki zisizodhibitika, unadhoofisha miundombinu ya kijamii kama ukosefu wa chakula, maji, uharibifu mkubwa wa mazingira, kukwamisha elimu, tiba, barabara na madaraja.

Afrika nzima ni majanga kuanzia pembe ya Afrika, eneo la Sahel hasa Mali, Sudan Kusini na Sudan kwenyewe hata Msumbiji itakumbukwa kulikuwa na mashambulizi ya uasi licha ya kwamba yamedhibitiwa.

### ATHARI KWA WOTE

Kukosekana kwa utulivu Uganda, DRC, Msumbiji, Sudan Kusini na Sudan, Ethiopia, Kenya ni hatari zaidi kwa Afrika Mashariki.

Hata hivyo bara lote si salama Ukanda wa Sahel wenye mataifa ya Burkina Faso, Cameroon, Chad, Gambia, Guinea Mauritania, Mali, Niger, Nigeria na Senegal kutokana na uasi na wanamgambo waasi kupigana ili kuchukua udhibiti hakuna zaidi mbali anguko la ustawi na maendeleo kutokana na ongezeko la wakimbizi kwa Afrika yote lakini hata kwenye nchi za Ulaya zinazopakana na bara hili.

Ikumbukwe ukimbizi unaongeza hofu na kusambaa silaha hasa bunduki zisizodhibitika, unadhoofisha miundombinu ya kijamii kama ukosefu wa chakula, maji, uharibifu mkubwa wa mazingira, kukwamisha elimu, tiba, barabara na madaraja.

Kuwepo kwa migogoro hiyo na uasi kunazidi kuumiza miundombinu ya kiuchumi ambayo tayari iko taabani kwenye nchi zote za Afrika.

Enzi za uhai wake Waziri wa Mambo ya Nje wa awamu ya nne, Bernard Membe, aliwahi kuushauri Umoja wa Afrika (AU) kuwa na kikosi kabambe cha kushughulikia na kukabiliana na migogoro, uasi na uvunjifu wa amani.

Alishauri kuwa wakati umefika wa kujipanga na kuwa na kikosi au kamandi iliyofunzwa, yenye vifaa, uwezo wa kufanya utafiti, wataalamu wa kijasusi na intelijensia na mbinu zote za kukabiliana uasi na mashambulizi badala ya kutegemea muda wote musaada wa Umoja wa Mataifa na nchi za Magharibi.

Ni vyema kuanzia sasa kufikiria wazo hilo ikiwezekana kila mara kuwaleta pamoja wachunguzi au majasusi, makachero kubadilishana ujuzi na utaalamu. Kushirikiana mbinu bora, kubainisha upungufu katika upelelezi ili kudhibiti vyema na kukwamisha shughuli na mashambulizi ya kigaidi na kiasi katika nchi zao.

Afrika mara nyingi inautegemea Umoja wa Mataifa na nchi za Magharibi kuingilia kati migogoro, uasi na vita vya wenyewe kwa wenyewe ijiulize hivi mazoea ya kuvitegemea vyombo hivyo yameleta mafanikio gani? Jibu lilete uelekeo mpya wa nini cha kufanya.

Licha ya AU, EAC na Umoja wa Mataifa baadhi ya vikosi vya SADC kukabiliana na waasi wa DRC wakimo ADF, M23 hatua hizo hadi sasa zimeshindwa kukomesha mashambulizi ya ADF kwa Uganda na DRC pia.

Waasi wa ADF wanadaiwa walianzisha uasi dhidi ya Rais Yoweri Museveni katika miaka ya 1990 kupinga utawala wake wakijijenga kutoka kambi ya awali katika Milima ya Rwenzori.

Kundi hilo lilishambuliwa na kudhibitiwa kwa kiasi kikubwa na wanajeshi wa Uganda lakini mabaki yalikimbia ndani misitu mikubwa ya mashariki mwa Kongo ambako wanadumisha uasi wakishambulia raia na majeshi nchini Kongo na Uganda.

JUKWAA LA VIONGOZI

WAZIRI MWIGULU NCHEMBA

# Anatisha jimboni anapobebwa juu juu asijikwae, wapigakura wakiri amefanya maajabu Iramba

•Walitumia njia za ng'ombe, leo wana barabara, amekomesha vibuyu mtoni kwa kusambaza maji

**Na Claudia Kayombo**

MIAKA 48 iliyopita Kijiji cha Makunda wilayani Iramba mkoa wa Singida, alizaliwa mtoto wa kiume kwenye familia ya baba Madelu Mhene na mama Asha Ramadhani, ndiye Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Mwalimu wake Godfrey Mitula, aliyemfundisha kuanzia la kwanza hadi saba, anasema Mwigulu ni wa sita kati ya watoto 11 kwa wazazi hao na kwamba alionyesha makeke ya kuwa mwanasiasa akiwa darasa la nne, mwaka 1990.

"Nakumbuka mwaka huo alikuja aliyekuwa mbunge wa Iramba Magharibi Nalaila Kiula, akapata mapokezi makubwa akitandikiwa nguo ili apite kutoka kwenye gari hadi jukwaani. Baada ya kuondoka Mwigulu aliniuliza hivi, 'mtu hadi awe mbunge inabidi asome hadi darasa la ngapi?"

Anasema akamjibu awe na elimu ya kutosha, lakini hakujua kama ndiyo ilikuwa mwanzo wa kupenda siasa na angefika alipofika leo.

Anaongeza kuwa wakati Kiula alikuwa akitandikiwa nguo katika ziara zake kijijini, Dk. Mwigulu anabebwa juu juu asikanyage chini.

Anafafanua kuwa mwanasiasa huyo kijana anayetokea familia ya wafugaji, wakati anamfundisha alikuwa mwepesi kuelewa na kuyashika anayofundishwa, mwenye adabu tena asiye na woga.

"Wakati mwingine anapochelewa shule tukimuuliza umechelewa wapi? Anajibu bila woga, nilikuwa nakamua maziwa,' anasema mwalimu Mitula.

Uwezo wake katika masomo yote ulidhihirika katika matokeo ya mtihani wa taifa wa la saba ambapo alichaguliwa kujiunga na Sekondari ya wenye vipaji maalum ya Ilboru.

Licha ya uwezo mkubwa wa kupokea anayojifunza, mwalimu wake anasema pia alikuwa na kipaji cha uongozi na kila alipokuwa na wenzake aliwaunganisha.

Mwalimu huyo anaongeza kuwa anajivunia kumfundisha Dk .Mwigulu ambaye hadi sasa anawajali na kuwapenda walimu wake. Tukikutana naye anapenda kuzungumza nasi Kinyiramba tena kwa furaha," anaeleza.

Yohana Msengi mmoja wa wazee wa kijiji hicho, anasema Dk. Mwigulu ni kijana aliyepewa kipaji cha kipekee kwani alikuwa ni mwenye huruma na upendo kwa wenzake tangu akiwa mdogo.

Msengi anasema ameyashuhudia makuzi ya Dk. Mwigulu, akiwa ana hudumu katika nyadhifa mbalimbali ikiwamo mwenyekiti wa kijiji cha Makunda anayesema mtunza hazina huyo wa serikali hakuwahi kupenda vurugu.

Kijana huyo aliyezaliwa baada kuundwa vijiji vya ujamaa, Msengi anamwelezea kuwa ameifanya Makunda upya na Iramba yenye maendeleo yasiyotarajiwa hapo awali.

"Wabunge wamepita wengi katika jimbo la Iramba lakini hayupo aliyejitahidi kufanya kazi hata japo nusu ya alizofanya Mwigulu. Kinamama walitembea na vibuyu kufuata maji vijiji jirani kilomita zaidi ya nane leo maji tunayo hapa kijijini, ametuletea mtoto wetu."

"Tangu uhuru barabara za kijiji hiki hazikuchongwa, tulikuwa tunapita njia za ng'ombe, sasa tuna barabara, zahanati, shule, amechukua watoto wa watu zaidi ya 2,000 katika jimbo hili anawasomesha kwa fedha zake." Anaongeza.

Anamsifu kwa kuwa chachu ya vijana wa familia nyingi kuzinduka katika lindi la ujinga na kupenda kusoma tofauti na ilivyokuwa hapo kabla kwa mujibu wa Msengi.

Nasema ukweli na wala simsifii bure, Mwigulu ameyafanya mengi ambayo watangulizi wake hawakutenda: "Ombi langu kwake atuboreshee barabara, aongeze maji katika kijiji chetu, zahanati yetu aifanye kuwa kituo cha afya ili hata huduma za upasuaji zipatikane hapa na atujengee chuo cha ufundi ili wanafunzi wanaomaliza sekondari wajifunze ujuzi hapa hapa," anasema mwenyekiti huyo mstaafu.

Nuhu Said mmoja wa vijana aliyekua pamoja na Dk. Mwigulu anasema wakati anasoma kidato cha tano aliwahi kuwakutanisha katika mkutano usio rasmi akawaambia kuwa ana dhamira ya kuibadilisha Makunda na Iramba kwa ujumla lakini hawakumwelewa.

Said anasema kwa kuwa Mwigulu alikuwa msomi pekee miongoni mwa wenzake, wapo walioona kuwa jambo analosema haliwezekani ila walimsikiliza tu.

"Wakati anagombea Rais Kikwete mwaka 2005 Mwigulu wakati huo alikuwa bado yupo shule, alipokuja likizo aliitisha mkutano katika bwawa la Makunda akatuambia kuwa tumuunge mkono Kikwete, huku akiahidi bwawa hilo angekuja kuliboresha.

Anaongeza kuwa mwaka 2010 Mwigulu alijitosa kutia nia ya kugombea ubunge miongoni mwa wazee tisa wenye uzoefu na masuala ya kisiasa akiwa wa 10, wapo walioamini kuwa asingewashinda, lakini aliwabwaga.

Wakati huo hakuwa na fedha wala gari katika mikutano yake alikuwa anatumbia wimbo "Namgulu, namgulu mpaka Dodoma. Wimbo wa Kinyiramba uliomaanisha atatembea kwa miguu hadi Dodoma kufikisha shida za wana Iramba na alishinda kweli.

Eliudi Elisha aliyesoma shule moja na kuchunga ng'ombe na Mwigulu anasema licha ya kuchunga walikuwa wakiwinda ndege pamoja mbugani, anasema alimtangulia moja akiwa la saba Waziri Mwigulu alikuwa la sita.

Elisha anabainisha kuwa elimu haikuwa imempa kiburi Mwigulu, alipokuwa anarudi likizo alikuwa anakwenda machungaji na daftari zake hadi mwisho wa likizo yake, huku akiwa na wenzake bila kubagua au kujikweza.

"Akiwa kidato cha tano alisema nataka kuibadilisha Iramba nzima, ukimtazama alikuwa na maono ya kuwa kiongozi mkubwa ambaye anaifundisha jamii umuhimu wa kuzingatia elimu," anasema Elisha.

Mwigulu ambaye ni mpenzi wa Yanga tangu mdogo, wakati anaanza harakati zake za kisiasa aliwaunganisha vijana kupitia michezo, anasema Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Makunda, Abel Shalua.

"Anapokuja haji kwa siri kama wanavyofanya baadhi ya viongozi, kutokana na tabia zake hata viongozi wa dini katika maeneo mbalimbali ya jimbo hilo wanawataka wana Iramba kumwombea," anasema.

Shalua anafafanua kuwa jambo la ajabu ni kwamba Dk. Mwigulu anafanya mambo mengi bila ubaguzi, yapo anayoyafanya zaidi katika maeneo mengine kuliko katika kijiji na kata aliyozaliwa.

Anamwomba Waziri Mwigulu kutia mkono wake katika ofisi ya kata, awatafutie wakulima masoko ya mazao yao kama alizeti, dengu, mahindi na maharagwe.

Akizungumzia utatuzi shida ya maji anasema:"Tulikuwa tunachota maji Kyengege kilomita 10 kutoka hapa Makunda, wakati mwingine tukiwa njiani tunajikwaa, yanamwagika na kurudi nyumbani mikono mitupu."

"Wajawazito walikuwa wanajifungulia njiani kwa kukosa zahanati, sasa aibu hiyo hatuna tena, zahanati tuliyojengewa hapa kijiji na mheshimiwa Mwigulu ipo," anasema.

Katibu wa machimbo ya dhahabu mgodi wa Sekenke One, Joseph Mnemba, anasema Dk Mwigulu amekuwa akiwaunga mkono kila wanapohitajia msaada wake.

"Wakati tunafuatilia kupata leseni ya Sekenke One, tulimfuata Dodoma, alitusaidia kila hatua hadi tukafanikiwa, kabla ya kupata leseni tulikuwa na hali mbaya sana. Januari mwaka huu tulikwenda tena kumweleza haja ya serikali kufanya uwekezaji wa kati badala ya huu mdogo unaofanyika sasa, akatuunganisha na Waziri wa Madini Dotto Biteko katika mchakato wa kufanikisha jambo hilo."

Katibu huyo anasema iwapo uwekezaji wa kati utaanza kazi katika mgodi huo ni dhahiri kuwa utakuwa na zana za kisasa ambazo zitaondoa maji ambayo ni kikwazo lakini pia mapato ya dhahabu yataongezeka maradufu.

Anafafanua kuwa hali iliyoko sasa machimboni hapo siyo nzuri kwa sababu wachimbaji wengi wanashindwa kuendelea na kazi katika mgodi huo ulioanza enzi za wakoloni wa Kijerumani.




Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba. **PICHA: MTANDAO**

> "Tangu uhuru barabara za kijiji hiki hazikuchongwa, tulikuwa tunapita njia za ng'ombe, sasa tuna barabara, zahanati, shule, amechukua watoto wa watu zaidi ya 2,000 katika jimbo...





## Wakazi Kondoa watakiwa kuchangamkia fursa barabara

**Na Ibrahim Joseph,** KONDOA

WANANCHI wa Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma, wametakiwa kuchangamkia fursa ya uwepo wa barabara kuu kwa kujenga vitega uchumi vikubwa ili kujikwamua kiuchumi.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wananchi na wanachama wa chama hicho kwenye mkutano wa hadhara wilayani humo.

Chongolo aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuchangamkia uwepo wa barabara kuu kutoka Misri hadi Afrika ya Kusini inayopita hapo kwa kujenga vitega uchumi vya biashara.

Alisema barabara hiyo inapitisha watu wengi hivyo wanatakiwa kujenga vitega uchumi karibu na barabara hiyo ikiwamo hoteli kubwa ambazo zitatoa huduma za chakula na malazi kwa wageni.

Aidha, alisema uwapo wa miradi hiyo itatoa ajira kwa wananchi wa wilaya hiyo na Watanzania wengine.

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Khamisi Mkanachi, alisema wamejipanga katika kuanza kuitumia fursa ya barabara hiyo kwa kutoa elimu ya biashara.

Mkanachi alisema kwa kutambua hilo Halmashauri ya Mji Kondoa wamejenga kituo kikuu kipya cha mabasi eneo la Bicha ili kunufaika na mapato ya ushuru wa mabasi na magari mengine yanayotumia kituo hicho.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanawajengea uwezo wananchi na wajasiriamali kuleta ushindani kwa kuwekeza kwenye maeneo yenye fursa za kiuchumi kwenye wilaya hiyo.

# Madiwani Singida wanaowasaidia w'biashara kutolipa kodi waonywa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MADIWANI wa Manispaa ya Singida wameonywa kuacha kuwa sehemu ya kuwasaidia wafanyabiashara kutokulipa kodi na ushuru kwa halmashauri, kwa kufanya hivyo kunazorotesha maendeleo, kukwama kwa miradi inayotekelezwa kwa kutegemea fedha za mapato ya ndani.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alitoa onyo hilo jana wakati wa kikao maalum cha Baraza la Madiwani wa Manispaa ya Singida kilichokuwa kikijadili hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa manispaa hiyo.

"Madiwani msiwe sehemu ya kufanya watu wasilipe kodi, nakumbuka wakati nimekuja hapa kuna watu walikuwa hawalipi 'service levy' mkubwa mmoja akaenda kunishtaki kwa waziri kwamba nawaonea wafanyabiashara lakini nilipompa ufafanuzi waziri jambo hili alibaki kushangaa na kucheka," alisema.

Aliongeza: "Unamtetea mtu ambaye anainyonya halmashauri, mtu unakuta anadaiwa Sh.milioni 30 anakuja anakula Sh.500,000 wewe unamtetea na kusema msipambane na mfanyabiashara wangu, msidanganyike kwa vitu vidogo vidogo."

Alisema halmashauri hiyo ina uwezo wa kukusanya fedha nyingi ukilinganisha na Sh.milioni 500 zinazokusanywa kwa mwezi, hivyo ni wajibu wa madiwani kuwasimamia wakuu wa idara ili kutekeleza majukumu yao.

"Wakati wangu nikiwa Singida kama kuna jambo tutagombana ni hoja za CAG kutofungwa, kutokusanya mapato na mji kuwa mchafu," alisema.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, alisema kinachosababisha hoja za ukaguzi ni katika matumizi ya fedha na kuwataka madiwani kwa kushirikiana na watendaji kuhakikisha wanazijibu hoja kwa wakati na kuzizalisha nyingine.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Daniel Chongolo, akizungumza wakati wa kikao cha nje na wakazi wa Kata ya Keikei, Kondoa mkoani Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wazazi zungumzeni na watoto kuwaepusha na ukatili'

**Paul Mabeja na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZAZI na walezi nchini wametakiwa kuzungumza na watoto wao na kufuatilia mienendo yao kila mara ili kuwaepusha na vitendo vya ukatili ikiwamo ubakaji, ulawiti pamoja na mimba za utotoni.

Takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2022, jumla ya matukio ya ukatili kwa watoto 12,163 yaliripotiwa ambapo kati ya hayo wavulana walikuwa 2,201 na wasichana 9,962 ukilinganisha na matukio 11,499 kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la matukio 664 kwa asilimia ya 5.8.

Ofisa Tarafa ya Farkwa, Mathias Kasuga, alibainisha hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika pamoja na ugawaji wa vifaa vya shule kwa wanafunzi 150 yaliyofanyika katika Kijiji cha Rofati Kata ya Gwandi Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma yaliyoratibiwa na Dorcas Aid Tanzania pamoja na Tunajali Development Initiatives.

Kasuga alisema watoto bado wanakabiliwa na kero ya ukatili wa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja ulawiti, ubakaji utumikishwaji katika ajira hatarishi, ndoa na mimba za utotoni.

"Vitendo hivyo vinaweza kumshawishi kufanya ngono au kubakwa, kulawitiwa na hata kuuawa pia watoto waheshimu wazazi, walezi na jamii, kufanya kazi na kutii maelekezo wanayopewa ili kuwa salama kwa ustawi wa maendeleo yao," alisema Kasuga.

Akizungumzia kauli mbiu katika maadhimisho hayo 'Zingatia Usalama wa Mtoto katika ulimwengu wa Kidigitali', Mratibu wa miradi ya watoto na wazee kutoka Dorcas Aid Tanzania Pamoja na Tunajali Development Initiatives, Goodluck Kivuyo, alisema waliamua kutumia kauli mbiu hiyo ili kuwakumbusha wazazi kutumia digitali bila kuathiri malezi ya watoto.

"Unakuta mtoto anaangalia filamu mzazi hafuatilii ile filamu inamaudhui gani hivyo kama wazazi watoe elimu kuhusu matumizi sahihi ya mitandao na mtoto apewe uhuru ili kuweza kufanya maamuzi pamoja na kujengewa uwezo ili kuelewa athari za mitandao," alisema Kivuyo.

Akisoma risala mwanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Msingi Rofati, Sarah Mathew, aliwataka viongozi wa dini kutoa elimu ya malezi na ndoa kwa wanandoa ili kupunguza migogoro inayosababisha kushindwa kulea watoto.

Mratibu wa kituo cha maendeleo ya mtoto na kijana Kijiji cha Rofati Wilaya ya Chemba, Ombeni Sifaeli, aliwataka wazazi kutoruhusu mtoto kutumia vifaa vya kielektroniki kama simu, intaneti na runinga ili kumwepusha kujiingiza kwenye maeneo hatari ya kufanyiwa ukatili wa mitandaoni.

Katika hatua nyingine, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Kongwa, Joseph Mshana, alisema serikali kushirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha kikosi kazi cha taifa cha kukabiliana na vitendo vya ukatili na ukiukwaji wa haki za watoto mitandao ili kuhakikisha wanatokomeza kabisa ukatili wa aina hiyo.

Pia mwezeshaji kutoka Shirika la World Vision, Pepetua Modestus, aliwaomba wazazi kuwafuatilia watoto wao juu ya usalama wa mtoto kidijitali kwa kuwa kuna baadhi ya watoto wanaangalia picha na video za ajabu kwenye vibanda umiza na kwenye simu za watu mbalimbali.





# TARI-Uyole yaanza 'vita' dhidi ya tindikali shambani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, kimeanza kushirikiana na wadau mbalimbali kukabiliana na tatizo la tindikali iliyokithiri kwenye mashamba.

Uwapo wa tindikali hiyo kunasababisha uzalishaji wa mazao mbalimbali katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kushuka.

Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti iliyofanywa na taasisi hiyo ni kwamba zaidi ya asilimia 14 ya ardhi inayofaa kwa kilimo katika mikoa ya ukanda huo imeathirika kwa kuwa na kiwango cha juu cha tindikali hali inayosababisha wakulima kukosa tija ya uzalishaji wa mazao.

Mtafiti wa Afya ya Udongo wa TARI Uyole, Fredric Mlowe, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya kwenye mkutano wa wadau mbalimbali wa kilimo uliokuwa na lengo la kuwasilisha taarifa ya ugunduzi wa chokaa ya kudhibiti tindikali hiyo.

Wadau walioshiriki kwenye kikao hicho ni wataalamu wa utafiti kutoka TARI, wataalamu kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na maofisa kutoka katika Kiwanda cha Saruji cha Mbeya ambacho ndicho kitazalisha chokaa hiyo.

Alisema hali hiyo inasababisha uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula kushuka kutokana na mazao hayo kushindwa kufyonza virutubisho vinavyowekwa kwa ajili ya kunenepesha mazao.

"Utafiti unaonyesha kwamba ekari moja ya mahindi mtu anatakiwa kuvuna tani tatu na zaidi lakini kiwango hicho katika mikoa yetu hakifikiwi kwa sababu mazao hayo yanashindwa kufyonza vizuri mbolea inayowekwa na hivyo nyingi inapotea," alisema Mlowe. Alisema njia pekee ya kupunguza tindikali hiyo ni kutumia chokaa ambayo kitaalamu inafanya kazi ya kufyonza tindikali kutokana na kuwa na madini ya kalsiamu ambayo yanashusha tindikali hiyo chini na hivyo kuchuja udongo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Juliana Mwakasendo, alisema baada ya kubaini hali hiyo kwenye udongo, wameanza kuhamasisha wananchi kutumia chokaa kupunguza tindikali hizo.

Alisema teknolojia hiyo ya kutumia chokaa ni muhimu na ikitumika ipasavyo itasaidia kupunguza tindikali hizo na kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula.

"Baada ya kukamilisha utoaji wa elimu tutaanza kusambaza chokaa hii kwa wakulima, tunaamini kwamba wakulima wetu wakihamasika kuitumia na wakafuata utaalamu wote hata uzalishaji wa mazao utaongezeka," alisema Dk. Juliana.

Alisema jukumu la kuzalisha chokaa hiyo na kuwafikishia wakulima, wamelikabidhi kwa Kiwanda cha Saruji cha Mbeya na wamekubaliana viwango vinavyotakiwa na kwamba wataendelea kufuatilia.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Khaled Ghareob alisema watahakikisha wanazalisha chokaa ya kutosha na kuisambaza kwa wakulima ili waendelee kuitumia kwenye mashamba yao na hivyo kukidhi malengo ya kupunguza tindikali.

Alisema mbali na kufanya biashara pia wanafanya kazi ya kuisaidia jamii kwa kuhakikisha wanawasaidia wakulima ambao ni sehemu ya jamii hasa kuwasaidia kwenye uzalishaji.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwenye hafla hiyo, Jaffari Haniu ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Rungwe aliwasisitiza wakulima kutumia teknolojia hiyo ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao.

Alisema matumizi ya chokaa hiyo ni sawa na kukarabati nyumba na hivyo akawataka wananchi kufanya hivyo ili kuongeza virutubisho kwenye udongo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na wananchi wa Kata ya Kabula katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe juzi alipokagua ujenzi wa Shule ya Msingi Ndembo ambayo imeanza kujengwa kwa nguvu za wananchi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wakulima mboga, matunda walia bidhaa kutotambulika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limetakiwa kutoa nembo ya ubora kwa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wa kiwanda cha kuchakata mboga na matunda cha Mbeya, ili bidhaa hizo ziaminike katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara kwenye kiwanda hicho kilichopo katika eneo la uwanja wa ndege wa zamani wa Mbeya.

Kiwanda hicho kimejengwa na shirika lisilokuwa la kiserikali linalojihusisha na hamasa ya kilimo cha mboga na matunda la HELVETAS ambalo ni miongoni mwa mashirika yanayotekeleza programu ya kuboresha mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani (AGRI-CONNECT) chini ya udhamini wa Umoja wa Ulaya (EU).

Homera alisema wajasiriamali kwenye kiwanda hicho wanazalisha bidhaa ambazo zinahitajika katika masoko mbalimbali lakini kutokana na kukosa nembo ya ubora hawawezi kuzipeleka.

"Hiki kiwanda ni kikubwa na kinawaunganisha wakulima, wasindikaji na wafanyabiashara, sasa TBS ni vizuri mkawawahishia nembo ya ubora ili bidhaa hizi ziwe na soko linalostahili," alisema Homera.

Mkurugenzi wa mradi wa KIBOWAVI ambao upo chini ya HELVETAS, Daniel Kalimbya alisema kiwanda hicho ni cha kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki na hivyo akawataka wasindikaji wengi kwenda kusindika bidhaa zao hapo ili kuongeza thamani ya mazao yao.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo mkubwa wa kuongeza ajira kwa wananchi lakini tatizo lililopo ni kukosekana kwa nembo ya ubora kutoka TBS ambayo ndiyo itawapa uhalali wajasiriamali hao kupeleka bidhaa hizo kwenye soko la nje.

"Hivi karibuni tuliwapeleka wajasiriamali wetu Malawi kwenye maonyesho ya viwanda, bidhaa zetu zilipendwa sana lakini tatizo ilikuwa ni kukosekana kwa nembo ya ubora kutoka TBS," alisema Kalimbya.

Mkaguzi wa TBS, Peter Namombo, alisema wanaendelea na utoaji wa nembo kwa wajasiriamali wanaozalisha bidhaa zao kwenye kiwanda hicho kulingana na namna wanavyokidhi vigezo.

# Serikali yaombwa kuwasaidia wajane wanaosomesha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wa vyuo vikuu mkoani Mbeya wameiomba serikali kuandaa utaratibu maalumu wa kuwasaidia wajane kusomesha watoto katika ngazi mbalimbali za elimu ikiwamo elimu ya chuo kikuu na vyuo vya kati ili kuwapunguzia mzigo.

Walitoa ombi hilo juzi kwenye maombi maalumu ya kuwaombea wajane ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kongamano la wajane nchini ambalo linatarajiwa kufanyika kitaifa jijini Mbeya Juni 23, mwaka huu.

Wanafunzi walioshiriki kwenye maombi hayo ni kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi (MCHAS) na wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya ambao walifanya maombi ya pamoja na wawakilishi wa wajane kutoka mikoa mbalimbali.

Maombi hayo yalifanyika katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya mahali ilipo Ndaki ya MCHAS ambapo wanafunzi hao walisema asilimia kubwa ya wajane hawana uwezo wa kuwasomesha watoto wao hasa katika ngazi ya chuo kikuu kutokana na uchumi wao kuwa mdogo.

Colnel Uzilo ambaye ni mwanafunzi wa MCHAS alisema ili kuwasaidia wajane hao, serikali inatakiwa kuanzisha utaratibu maalumu wa kuwasomesha watoto wanaotokana na familia hizo za wajane ili na wao wapate haki yao ya kupata elimu.

Alisema watoto wengi wa wajane wengi huwa wanakuwa na ndoto ambazo huwa wanahitaji kuzifikia lakini zinaanza kupotea wanapokuwa hususani wanapompoteza mzazi mmoja hasa ambaye alikuwa ndiye mtafutaji mkuu wa familia.

Naye Nuru Mwamli ambaye ni mwanafunzi wa Chuo cha Mzumbe, alisema kundi la wajane linatakiwa kuwezeshwa mitaji ili kuwa na uwezo wa kujikimu kiuchumi na kuwa na uwezo wa kulea familia ambazo wanakuwa wameachiwa na wenza wao.

Alisema baadhi ya wajane huwa wanaporwa mali zao baada ya waume zao kufariki jambo ambalo linawafanya waishi maisha magumu na kushindwa kulea familia.

Alisema kundi hilo linahitaji pia msaada wa kisheria ili kuokoa mali zao ambazo wanakuwa wameachiwa na wenza wao kwa maelezo kuwa mali hizo zikiokolewa zitawasaidia wajane hao kulea familia zao vizuri.

Mwakilishi wa Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha MCHAS, Linus Michael, aliiomba serikali kuwasaidia wajane hao kwa kuwaunganisha kwenye vikundi vya ujasiriamali na kuvikopesha mitaji ambayo itawasaidia kuendesha maisha ya familia zao.

Alisema kundi hilo linatakiwa kuwa miongoni mwa makundi yanayonufaika na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) pamoja na mikopo inayotolewa na halmashauri kwa wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Baadhi ya wajane walioshiriki ibada hiyo walisema wanahitaji misaada mbalimbali kutoka serikalini na kwa wadau wengine kwa ajili ya kuendesha maisha ya familia zao.

Mmoja wa wajane hao, Nuru Kalekenya alisema wajane wengi wanalea watoto ambao wengine ni wa waume zao pamoja na wajukuu lakini uchumi wao ni mdogo na hivyo wanapata wakati mgumu kuzihudumia familia hizo.

Aliiomba serikali kuwasaidia mitaji ili na wao waingie kwenye biashara ambazo zitawasaidia kupata kipato cha kuendeshea maisha yao.





## Serikali kuikarabati gati ya kisiwa cha Tumbatu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema gati ya kisiwa kidogo cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja itafanyiwa matengenezo ili kuruhusu meli ndogo pamoja na majahazi kutia nanga na kushusha bidhaa na mizigo ya wananchi.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdulatif Yussuf, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Wingwi, Kombo Mwinshehe aliyetaka kujua lini gati ya Kisiwa cha Tumbatu itafanyiwa ukarabati na kutoa huduma kwa wananchi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Nadir alikiri gati ya Tumbatu kuchakaa akisema haiwezi kutoa huduma za ufanisi kwa wananchi katika shughuli za usafiri kwa wananchi wa eneo hilo na maeneo mingine.

Alisema Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano imejipanga kuzifanyia ukarabati gati ndogo ambazo ni muhimu katika kutoa huduma kwa wananchi katika maeneo ya visiwa vidogo.

Alisema katika Kisiwa cha Tumbatu gati iliopo imejengwa zaidi ya miaka 10 ambayo haikidhi tena mahitaji ya kutoa huduma kwa wananchi pamoja na kupokea bidhaa.

Aidha, alizitaja gati nyingine ambazo zimeingizwa katika mpango wa ukarabati ni Kisiwa Panza Mkoa wa Kusini Pemba ili kuruhusu wafanyabiashara wanaotoka sehemu nyingine kutia nanga na kushusha bidhaa.

**Alisema Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano imejipanga kuzifanyia ukarabati gati ndogo ambazo ni muhimu katika kutoa huduma kwa wananchi katika maeneo ya visiwa vidogo.**

# ‘Wasimamizi wa sheria imarisheni ulinzi, mfumo wa Mahakama’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Baraza la Watoto Mkoa wa Kusini Unguja, Minna Amour Haji, amesema taasisi zinazosimamia mwenendo wa masuala ya sheria zinapaswa kuimarisha hatua ya ulinzi na mfumo wa Mahakama ili kupunguza mzigo wa ushahidi kwa wasichana katika kesi za udhalilishaji.

Alitoa wito huo juzi katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika visiwani Zanzibar ambayo yaliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA, Zanzibar).

Alisema bado mwenendo wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia unachukua muda mrefu hadi kukamilika kutokana na kuwapo kwa taasisi nyingi zinazoshughulikia mwenendo wa kesi hadi kutajwa mahakamani.

Haji alisema ipo haja ya kuwapo kwa kasi ya kufanya upelelezi na kukamilisha kwa ajili ya kufikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na yeye kuipeleka mahakamani kwa ajili ya kusomwa.

Alisema mchakato wa kufunguliwa kwa kesi mahakamani unachukua muda mrefu kiasi cha kuwavunja moyo wazazi na wengine kufika wakati wa kuanza kufanya mazungumzo na wahusika kwa ajili ya kuyamalizia kienyeji.

"Mchakato wa kesi za udhalilishaji bado unachukuwa muda mrefu licha ya kuwapo kwa juhudi za makusudi ikiwamo kuanzishwa kwa Mahakama ya Watoto Zanzibar," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya Kimtandao kutoka Jeshi la Polisi Zanzibar, Issa Mohamed Salum, alisema hali ya udhalilishaji makosa ya kimtandao ni mbaya na wanawake ndiyo waathirika wakubwa.

Alisema hali ya ukatili na udhalilishaji wa kupitia teknolojia ya kimtandao sio nzuri kwa sababu watumiaji wengi wa mitandao ya kijamii hawajui sheria na kanuni na taratibu za matumizi salama ya kimtandao.

"Wakati umefika jamii inatakiwa itumie vizuri na salama mitandao ya kijamii ili kuepuka kubanwa na sheria bila ya kujijua, huu ni wakati wa kutumia simu kwa ajili ya kuchambua fursa za maendeleo ya kiuchumi na elimu," alisema.

Naye Mkuu wa Dawati la Jinsia, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Salum Khamis Machano, alisema matumizi ya teknolojia kwa watoto na wanafunzi kwa sasa hayaepukiki lakini elimu zaidi inahitajika ili yatumike vizuri kwa wakati sahihi.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi limefanya maboresho makubwa katika madawati yake yote yaliopo katika vituo vya wilaya kwa ajili ya kuona yanaongeza ufanisi wa kazi na kuleta matokeo mazuri.

Mwenyekiti wa Mahakama za Watoto, Zuwena Abdulkadir, alitaka kuwapo kwa matumizi sahihi ya kidijitali katika matumizi ya mitandao ikiwamo simu, kwamba utafiti unaonyesha baadhi ya watoto wanaofikishwa mahakamani wanapoulizwa kwa nini wamefanya vitendo hivi wanajibu kwamba wameona katika mitandao.

Alisema wakati umefika watoto watumie mitandao ya kidijitali ya simu kwa kupata idhini ya wazazi wao katika maeneo maalumu ya ufafanuzi wake.

"Vitendo vingi vya udhalilishaji wa kijinsia watoto kwa watoto wanafanyiana baada ya kuviona kupitia mitandao ya kijamii ikiwamo simu," alisema.

Akiwasilisha ripoti inayohusiana na ulinzi wa mtoto, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Sikujuwa Omar, alisema marekebisho na mapitio ya sheria mbalimbali zinazomlinda na kumhusisha mtoto zinahitaji kupitiwa upya.

"Marekebisho ya sheria mbalimbali zinazomlinda mtoto na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia zinahitaji kurekebishwa haraka kwa ajili ya kuhakikisha mtoto anakuwa salama zaidi ikiwamo na matumizi ya mawasiliano ya teknolojia ya simu," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya TAMWA - Zanzibar, Asha Abdi, aliwataka wazazi kuishi karibu na familia zao ikiwamo watoto na kuangalia mwenendo wa maisha yao ya kila siku.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mysol, Godfrey Mugambi, akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa duka jipya la vifaa vya umeme wa jua na huduma za kampuni hiyo Zanzibar jana. Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamu wa Rais kufunga mradi wa jenga amani yetu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Maosud, anatarajia kufunga mradi wa jenga amani yetu Juni 27, mwaka huu.

Mradi huo uliokuwa ukifadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) umedumu kwa miezi 19, kwamba siku ya kuhitimishwa unatarajiwa kuhudhuriwa na washiriki 200 ambao ni wanufaika kutoka vyama vinne vya siasa ikiwamo CCM, ACT-Wazalendo, CUF na CHADEMA.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu hafla hiyo, Mratibu wa mradi huo, Almasi Mohammed, alisema mradi huo ulioanza mwanzoni mwa mwaka jana, ulilenga kuchangia usuluhishi wa migogoro ya kisiasa na ustawi wa Zanzibar.

"Mradi huu unatekelezwa ukiwa ni mwitikio wa uzoefu wa migogoro ya kisiasa iliyodumu kwa muda mrefu na hali ya vurugu ambayo imekuwapo zaidi katika nyakati za uchaguzi," alisema.

Alisema hali hiyo iliathiri ustawi wa jamii na kusababisha uwepo wa mradi huo ili kuchangia juhudi nyingine zilizofanywa na wadau.

"Mradi huu wa amani yetu, mshikamano wetu umefanya mambo kadha kwa kadha ambayo yalihusu kujenga uelewa kwa watendaji wa kisiasa kupitia mafunzo ya kuwajengea uwezo na kuwashirikisha katika mazungumzo ili kuimarisha mahusiano ya kuaminiana hasa katika vyama vya siasa," alisema.

Aidha, alisema timu ya mradi inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika utekelezaji wa mradi huo akiwamo Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ofisi ya Mufti, Mrajis wa Asasi za Kiraia, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, vyama vya siasa na waandishi wa habari.

Hata hivyo alisema miongoni mwa mafanikio yaliopatikana katika mradi huo ni maridhiano ya kisiasa visiwani Zanzibar na kuimarika kwa hali ya amani na usalama na kuondosha tofauti za kisiasa kwa wananchi.

Mradi huo umefadhiliwa na EU kwa kushirikiana na Taasisi ya Konrad Adenauer Stiftung (KAS) na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) na uligharimu Sh. bilioni 1.5.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**PATRICK JAMES NYANGUBHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba: **S0140-0601** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MZUMBE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2017**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: 9910837283827**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA**
**KITUO CHA KARABAGAINE**
**SHAURI LA TALAKA NO. 05/2023**
**DERIA ARCHELAUS .........MDAI**
**DHIDI YA**
**DAVID CATHBERT............MDAIWA**

**DAVID CATHBERT** unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii tarehe 19/07/2023 saa 08:30 asubuhi kuja kujibu madai ukiwa na mashahidi wako.

Kwa kuwa ni siku ya kusikiliza shauri fika na hati zote zinazohusiana na shauri hili na kama hautahudhuria shauri hili litaendelea kusikilizwa upande mmoja.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 19 Juni 2023.

.............................................
**C. R. RICHARD**
**HAKIMU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARABAGAINE.**

**IN THE REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF ARUSHA**
**AT ARUSHA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION 13 OF 2023.**
**PROLIMINA JUMA MTEY PLAINTIFF/APPLICANT/D/HOLDER**
**VERSUS**
**FEBRONIA JUMA MTEY**
**DEFENDANT/RESPONDENT/J/DEBTOR**
**NOTICE OF MENTION**

**TO:FEBRONIA JUMA MTEY**
**TAKE NOTICE** that tje above case has been fixed for mention in the District Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the 6day of 7 2023 at 9:00am O'clock in the forenoon.

You may appeal in person or by Advocate or agent duly authorized to appeal on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

TAKE FURTHER NOTICE That in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence.

GIVEN under my hand and the seal of the court this 20 day of 6 2023.

DISTRICT MAGISTRATE I/C
ARUSHA

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**BARAKA MWAKITWANGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye Jina la **DIAMOND MOTORS LIMITED**, namba za usajili **T 462 AVS** aina ya **MITSUBISHI,** Chasis **No.MMBJNKB408D074165.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Taarifa ya polisi **MWA/NYA/RB/206973/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENJAMINI MADUKANI MWINULA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 520 DDN aina ya TOYOTA- IST,** Chasis **No.NCP600038514.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Taarifa ya polisi **MWA/NYA/RB/206978/2023**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MWANZA**
**SHAURI LA MADAI YA ARDHI NA 17 YA 2023**
**SAMWEL MAKOYE MIHAYO.........MUOMBAJI 1**
**YOHANA JACKSON.....................MUOMBAJI 2**
**DHIDI YA**
**GERALD YUSUPH.........MJIBU MAOMBI 1**
**VEDASTUS J MSHOLA.........MJIBU MAOMBI 2**
**DISMAS MAYUNGA MAGESA.........MJIBU MAOMBI 3**
**GRESI ENOS............MJIBU MAOMBI 4**
**EDINA JONATHAN SAYI KAMINI.........MJIBU MAOMBI 5**
**STELLA MISILIKALE MAGESA .........MJIBU MAOMBI 6**

**Kwa**
**GERALD YUSUPH**
**VEDASTUS J MSHOLA**
**DISMAS MAYUNGA MAGESA**
**GRESI ENOS**
**EDINA JONATHAN SAYI KAMINI**
**STELLA MISILIKALE MAGESA**
**POPOTE WALIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Fahamu kwamba, shauri tajwa hapo juu ambalo wewe ni mjibu rufaa namba 2 limepangwa kusikilizwa mbele ya mahakama hii tarehe 03/07/2023 saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mh Jaji N.N KILEKAMAJENGA

Hivyo manatakiwa kuhudhuria mahakamani wewe wenyewe au mwakilishi wako siku hiyo bila kukosa kutohudhuria kwako kutaifanya mahakama hii iendelee na shauri hili bila wewe kuwepo

Imetolewa kwa amri na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 06 mwezi juni, 2023

**NAIBU MSAJILI**
**MWANZA**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SUBIRA A. NYAMADYAKI,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha **Diploma** chenye Index namba **0506013484** kilichotolewa na **Dar es Salaam Institute of Technology** mwaka **2009**. na cheti cha Barchelour chenye Index namba **0906026438** kilichotolewa na **Dar es Salaam Institute of Technology** mwaka **2012**

Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/330955/2022.**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**
**MISC. CIVIL APPLICATION NO. 7 OF 2023**

**SAKAYA KISAIRO SHERU....................APPLICANT**
**VERSUS**
**JONAS JAMES MSAGANZI................RESPONDENT**

### NOTICE OF DATE MENTION

THE NOTICE that the above named case has been fixed for Mention on the 23rd day of June, 2023 at 08:30 am Before Hon. L .B. Lyakinana - PRM

YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

Given under my hand and the seal of the Court this **13th day of June , 2023**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO

## NAFASI YA KAZI

KAMPUNI YA MADAWA ILIYOPO DAR ES SALAAM INATAFUTA SALES MAN. AWE ANAJUA KUENDESHA PIKIPIKI NA AWE NA LESENI.

PIGA SIMU NAMBA: +255 713 786 300

## TANGAZO LA MNADA

**JOFORTE AUCTION MART COMPANY LTD** Kwa niaba ya Benki ya CRDB, Tunatoa taarifa kwa wadaiwa/wadhamini wafuatao kulipa madeni yao yote wanayo daiwa na benki hiyo kuwa ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya tangazo hili, Iwapo watashindwa kufanya hivyo tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana zao kama inavyo onesha kwenye jedwali hapa chini.

| S\N | JINA LA MDAIWA\MDHAMINI | DHAMANA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | JOSIA GERALD LUHUNGA | KIWANJA NA 263, KITALU 'G' ENEO LA ILOLO, MPWAPWA | 18\07\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 2. | ZEPHANIA EMANUEL NGOGO | DHAMANA ILIYOPO KWENYE KIWANJA KISICHOPIMWA ENEO LA LUKOBE, MANISPAA YA MOROGORO. | 12\07\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 3. | ABDALLAH KIBWANA KELEMJI | DHAMANA ILIYOPO KWENYE KIWANJA KISICHOPIMWA ENEO LA RUHEMBE – MADUKANI, WILAYA YA KILOSA. | 14\07\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |

**Masharti ya Mnada.**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
4. Gharama zote za kubadili hatimiliki ni za mnunuzi
5. Gharama za umiliki na kumtoa mwenye dhamana ni za mnunuzi
6. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0659706393 / 0734232220**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**LAKATO SAFARIS LIMITED**
**P.O.BOX 7337**
**ARUSHA - TANZANIA**
**THE COMPANIES ACT { CAP 212 R.E 2002}**
**CALL FOR A FINAL GENERALMEETING OF LACATO SAFARIES LIMITED COMPANY NUMBER 138889**
**(Made under section 345 of the Companies Act [CAP 212 R.E 2002])**

Where **LAKATO SAFARIS LIMITED** is a company limited by shared incorporated under the Companies Act [ cap 212 R . E 2002], with its registered office located at House No. 3, Lowasa street, Sakina Arusha which is duly registered by the Registrar of Companies with present two shareholders.

Whereas, on **28th day of February 2023** passed a special resolution to wind up its afairs and **Mr. PETRO ROBERT KITINGALLA** was appointed as the Liquidator for the purpose of winding up the affairs and distributing the assets of the Company

Therefore, it is from thet capability, the Liquidator calls for a General Meeting of the Company on **14th day of April 2023** for the purpose of laying before it the account and giving all other relevant explainations relating to the winding up of the affairs and distributing the assets of the Company thereto.

Dated at Arusha this **20th** Day of **March, 2023**

Liquidator

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Russia yatembeza kipigo kila mji muhimu Ukraine

**KYIV, Ukraine**

SIKU chache baada ya jopo la viongozi wa Afrika kujaribu kumaliza vita ya Ukraine, Russia imefanya mashambulio makali kwa kutumia ndege zisizo na rubani na kulenga miji muhimu ya Kyiv, lviv na Zaporizhia.

Taarifa kutoka nchini Ukraine, zilisema jeshi la wanahewa la Ukraine limehesabu zaidi ya ndega 35 zisizo na rubani zilirushwa na zote isipokuwa tatu ziliharibiwa.

Hakuna mtu aliyejeruhiwa katika shambulio la Lviv.

Lakini mkuu wa mamlaka ya Lviv, Maksym Kozytskyi, alisema maeneo muhimu matatu yalioshambuliwa yalifikiwa na ndege zisizo na rubani za Shaheed za Iran na kulipua baadhi ya majengo.

Zaidi ya ndege zisizo na rubani 20 zilirushwa katika mji mkuu kwa mpigo kutoka eneo la Urusi kuelekea kaskazini na kutoka pwani ya Bahari ya Azov, kusini-mashariki, kulingana na jeshi la anga.

Mamlaka ya Kyiv ilisema hilo lilikuwa tukio la kwanza ndani ya siku 18.

Maofisa wa kijeshi walisema, Zaporizhzhia ilishambuliwa na idadi ya makombora ya balestiki ya Iskander-M.

Ndege tatu zisizo na rubani pia zilidunguliwa katika eneo la kusini la Mykolaiv, gavana huyo alisema.

Eneo la Zaporizhzhia ndilo kitovu cha mashambulizi mengi ya sasa ya jeshi la Ukraine ya kujaribu kukomboa maeneo yaliotekwa na Russia mwanzoni mwa uvamizi wake kamili mnamo Februari 2022.

Naibu Waziri wa Ulinzi, Hanna Malyar, alisema saa chache vikosi vya Ukraine vilifanikiwa kukikomboa kijiji cha Piatykhatky walipokuwa wakijaribu kuvunja mstari wa mbele wa majeshi ya Russia katika eneo la kusini.

Alisema kilikuwa kijiji cha nane cha Ukraine kutekwa tena katika wiki iliyopita. Hakuna taarifa za uthibitisho huru zilizotolewa kuhusu mapigano hayo.

Katika hotuba yake ya kila siku kwenye runinga ya usiku, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alisema kuwa katika baadhi ya maeneo wanajeshi walikuwa wakisonga mbele huku katika maeneo mengine wakishikilia misimamo yao dhidi ya mashambulizi ya Russia.

Waziri wa ulinzi, alisema msukumo wa Ukraine umesonga mbele kiasi cha kilomita saba sawa na maili 4.3 katika njia mbili huko Zaporizhzhia, kuelekea miji inayokaliwa ya kusini ya Melitopol na Berdyansk.

Meya aliyehamishwa wa Melitopol, Ivan Fedorov, alisema wakazi wameona vikosi vya Russia vikiondoka eneo la Kherson magharibi zaidi kuelekea mstari wa mbele huko Zaporizhzhia.

Melitopol na Berdyansk ziko kwenye njia ya pwani kutoka Russia hadi Crimea inayoonekana kuwa muhimu kwa jeshi la Russia kwa sababu daraja la Mlango wa Bahari wa Kerch kutoka nchini humo hadi Crimea.

Mbunge wa Urusi alisema mapema mwezi huu kwamba daraja hilo halikuzingatiwa kuwa salama lakini "ukanda wa ardhini" ulikuwa unafanya kazi kama kawaida.

Maofisa wa kijasusi wa nchi za Magharibi wanasema wanajeshi wa Russia wameondoka kwenye mstari wa mbele wa Kherson katika maeneo ya karibu na mto Dnipro baada ya kujaa maji kufuatia bwawa la Kakhovka kuharibiwa Juni 6, mwaka huu.

**BBC**



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Mpondwe nchini Uganda wakishiriki mazishi ya mmoja wa wanafunzi waliouawa katika Shule ya Sekondari ya Lhubiriha, baada ya waasi kuvamia na kuchoma moto mabweni na kuua wanafunzi 42. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Tunubu awatumbua wakuu wa jeshi

**ABUJA, Nigeria**

RAIS wa Nigeria, Bola Ahmed Tinubu, amewafuta kazi wakuu wa usalama wa nchi hiyo katika mabadiliko makubwa katika majeshi ya nchi hiyo.

Waliotenguliwa katika majukumu yao ni mkuu wa ulinzi, mkuu wa jeshi la majini na mkuu wa kikosi cha anga, ambao wote walistaafishwa na nafasi zao kuchukuliwa na maofisa wapya.

Taarifa rasmi ilisema Rais Tinubu ameidhinisha kustaafu mara moja kwa wakuu wote wa polisi akiwamo inspekta Jenerali wa polisi, washauri, mdhibiti mkuu wa forodha.

Rais Tinubu pia amevunja bodi za taasisi zote za serikali, lakini hakujumuisha zingine zikiwamo baraza la mahakama, baraza la uchaguzi na tume ya huduma ya polisi.

Mabadiliko hayo katika idara za usalama yanajiri wiki mbili baada ya kiongozi huyo kukutana na wakuu wa usalama na kuwaamuru kufanya kazi kwa pamoja ili kukabiliana na changamoto za ugaidi, uasi, ujambazi, wizi wa mafuta na uharamia.

Nigeria imekuwa ikikabiliwa na wimbi la mashambulizi yanayodaiwa kufanywa na makundi ya kijihadi na magenge mengine ya wahalifu, wakiwamo majambazi ambao hujihusisha zaidi na utekaji nyara ili kujipatia fidia.

Kumekuwa na miito ya mara kwa mara kutoka kwa mashirika ya kiraia wakati wa serikali iliyopita kutaka wakuu wa usalama wabadilishwe kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kukabiliana na hali hiyo.

**BBC**

# China, Marekani zakubaliana utulivu

**BEIJING, China**

NCHI za China na Marekani zimekubaliana kuleta hali ya utulivu katika ushindani wao na kuepuka kutumbukia katika mzozo utakaosababisha vita baridi.

Hata hivyo, mataifa hayo yameshindwa kuafikiana kuhusu mambo muhimu ikiwa ni pamoja na mahusiano ya kijeshi.

Wakati akikamilisha ziara yake nchini China, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alikutana kwa mazungumzo na Rais wa China Xi Jinping, na wawili hao wamekubaliana kurejesha mahusiano mema kati ya mataifa hayo ambayo kwa muda yamekuwa yakizozana.

Blinken alimaliza ziara yake huku ombi lake kuu la kutaka kurejesha mawasiliano ya kijeshi likikataliwa na China. Marekani inayapa umuhimu mahusiano hayo ya kijeshi ili kuepuka migogoro hususan kuhusu Taiwan.

Marekani na China pia zimeshindwa kufikia makubaliano kuhusu masuala kadhaa huku kila upande ukionekana kusalia na msimamo wake hasa kuhusu masuala ya kibiashara, mzozo wa Taiwan, haki za binaadamu huko China na Hong Kong na hata uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Blinken alisema aliibua wasiwasi wake kuhusu namna China inavyowatendea watu wa jamii ya wachache wa Uyghur.

Viongozi hao walisisitiza umuhimu wa kuwa na uhusiano thabiti kati ya nchi hizo mbili na kusisitiza kuwa mzozo wa aina yoyote kati ya mataifa hayo unaweza kusababisha matatizo makubwa kimataifa.

**DW**

**Marekani na China pia zimeshindwa kufikia makubaliano kuhusu masuala kadhaa huku kila upande ukionekana kusalia na msimamo wake hasa kuhusu masuala ya kibiashara, mzozo wa Taiwan, haki za binaadamu huko China na Hong Kong na hata uvamizi wa Russia nchini Ukraine.**

HABARI MICHEZO

# MASHUJAA YATAMBA KWENDA KUIDUWAZA TENA MBEYA CITY

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mashujaa FC ya Kigoma imeahidi kuishangaza tena Mbeya City nyumbani kwao wakati wa mechi ya marudiano ya 'play off', itakayopigwa kesho kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Meja Mstaafu, Abdul Mingange, amesema soka lililochezwa juzi kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, ndilo litakalokwenda kuchezwa Uwanja wa Sokoine Mbeya, akiweka wazi dhamira ya timu hiyo na wakazi wa Kigoma kutaka kuiona Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

**Mashujaa iliichapa Mbeya City mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika katika mechi ya kwanza ya 'play off' kwa mabao ya Abiud Mtambuka dakika ya 24, Asanga Stalon (dk. 69) na Shadrack Ntabindi (dk. 78) kwa mkwaju wa penati wakati goli la kufutia machozi la Mbeya City likiwa ni la kujifunga kupitia kwa Aziz Sibo dakika ya 63.**

"Tulistahili kushinda na kuna watu wana wasiwasi kuwa labda tutakwenda kupoteza Mbeya kwa sababu mechi ya kwanza ya 'play off' dhidi ya Pamba tulishinda mabao 4-0, lakini tukaenda kuruhusu mabao 4-1, bao moja la ugenini likatuvusha, lakini kwa hili nawahakikishia tunakwenda kuwashangaza huko huko kwao, hii timu yangu ina uwezo wa kupata bao ugenini, tukifanikiwa kufunga tu huko bao moja au zaidi, tayari ndoto zetu zitakuwa zimetimia," alisema Mingange ambaye alikuwa akiifundisha pia timu ya Mbeya City, na Ndanda FC.

Mashujaa iliyokuwa Ligi ya Championship, ilifanikiwa kufika hatua hiyo baada ya kuiondoa Pamba kwenye mechi ya mchujo kwa jumla ya mabao 5-4, sasa inatakiwa kushinda, kupata sare au kufungwa bao lisilozidi moja ili kupanda Ligi Kuu, ikiifuata JKT Tanzania na Kitayosce ambayo kwa sasa imebadilishwa jina na kuitwa Tabora United.

Kwa upande wa Mbeya City, hii ni mara ya pili kucheza 'play off', msimu wa 2019/20 ilicheza dhidi ya Geita Gold wakati huo ikiwa Championship, lakini ilifanikiwa kubaki kwa jumla ya mabao 2-1, kwa sare ya bao 1-1 ugenini na kushinda 1-0 nyumbani, Mbeya.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, ameahidi kutoa usafiri kwa mashabiki wa soka mkoani humo kwenda jijini Mbeya kuipa hamasa na kushangilia Mashujaa FC, baada ya kufurahishwa na ushindi, lakini umati uliojitokeza na kushangilia kwa aina yake.

UZINDUZI...



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Ladislaus Matindi (wa pili kushoto), Waziri Mstaafu, Mary Nagu (kushoto), Paroko wa Parokia ya Mtakatifu Petro Oysterbay, Alista Makubi (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa Kamati ya Waleyi Parokia ya Mtakatifu Petro, Edwin Sanda, wakikata keki ikiwa ni sehemu ya uzinduzi wa albamu ya pili ya Kanuni ya Dhahabu ya Kwaya ya Mtakatifu Cecilia Oysterbay, hafla hiyo ilifanyika Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JKT Tanzania na mkakati wa usajili

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Timu ya JKT Tanzania umeweka wazi kuwa Ijumaa wiki hii wataanza rasmi mchakato wa kupitia mapendekezo ya wachezaji walioainishwa katika ripoti ya kocha Hamsini Malale kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu wa 2023/24 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tetesi zilizopo ni kwamba, baadhi ya majina ya wachezaji ambao wanatajwa kuwaniwa ndani ya timu hiyo ni pamoja na winga wa zamani wa Simba, Hassan Dilunga, Ismail Aziz Kader kutoka Azam FC na Deusdedith Okoyo wa Geita Gold FC.

Taarifa zinadai tayari nyota hao wameshamalizana na uongozi wa timu hiyo kwa kusaini mkataba wa miaka miwili kila mmoja tayari kukitumikia kikosi hicho kilichorejea tena Ligi Kuu kikitokea Championship.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Speratus Lubinga, alisema wametoa majukumu ya usajili kwa benchi la ufundi linaloongozwa na Malale ambalo limependekeza baadhi ya nafasi ili kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Bara.

Alisema wanatarajia Ijumaa wiki hiii kuanza mchakato wa kupitia majina yote yaliyopendekezwa ikiwamo nyota hao wanaotajwa kabla ya kuingia nao makubaliano rasmi kuelekea msimu ujao.

"Usajili tulianza nao mapema kipindi ambacho tuko Ligi ya Championship, tulianza kutengeneza timu yetu huko na baada ya kucheza Kombe la Shirikisho (FA Cup) na timu za Ligi Kuu, kocha Malale ameona mapungufu yetu na ni aina gani ya wachezaji ambao tunahitaji kuwasajili iwe ndani au nje ya taasisi," alisema.

Kwa upande wa Kocha Malale, alisema ameshakabidhi ripoti ambayo imeeleza aina ya wachezaji anaowahitaji kwa viongozi wao, hivyo wanachosubiri ni dirisha la usajili lifunguliwe.

"Katika usajili maeneo yote matatu ambayo ni ulinzi, kiungo na ushambuliaji tutasajili, lakini kwa sasa siwezi kusema ni kina nani, dirisha likifunguliwa tutafanya usajili ambao utaleta ushindani katika Ligi Kuu," alisema Malale.

## Namungo kusajili wapya wanne tu

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Namungo FC limesema linatarajia kuongeza wachezaji wanne kwa ajili ya kuiongezea nguvu timu hiyo kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Denis Kitambi, alisema ataongeza washambuliaji watatu pamoja na beki mmoja.

"Nafasi hizo ndizo ambazo zilikuwa na mapungufu msimu uliopita, malengo yangu ni kuwa na kikosi bora," alisema Kitambi.

Kocha huyo alisema tayari wameanza kufanya mazungumzo na baadhi ya wachezaji ambao wanawahitaji na kwamba muda wowote kuanzia sasa watamalizana nao. Alisema wachezaji ambao atawasajili wanatoka kwenye klabu kubwa hapa nchini na baadhi nje ya nchi.

"Malengo yangu ni kufanya vema msimu ujao na kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ninapaswa kufanya maandalizi mapema," alisema.

Akizungumzia msimu uliopita alisema ulikuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa kwani kila timu ilikuwa inacheza kwa ushindani jambo ambalo linawafanya wazidi kujizatiti zaidi kuelekea msimu ujao wa 2023/24.

## Korosho Queens yafuzu Taifa Wavu

**Na Frank Monyo**

KLABU ya Wasichana ya Mpira wa Wavu ya Korosho Queens ya mkoani Mtwara, imefuzu kushiriki Ligi ya Taifa ya Mpira wa Wavu Tanzania (TVNL), kwa msimu wa 2023 inayotarajia kuanza Juni 26, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Korosho Queens ni moja kati ya klabu 10 za wanawake zitakazoshiriki ligi hiyo itakayofanyika katika viwanja vya Gwambina zamani TCC Klabu Chang'ombe, kwa mtindo wa mizunguko minne.

Meneja wa Klabu ya Korosho Queens, Hussein Kibombwe, ambaye ni Mkufunzi wa Chuo cha Ualimu Mtwara, alisema: "Tumeanzisha Klabu ya Korosho Queens ili kuendeleza vipaji vya wasichana mahiri wanaopatikana kupitia mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA pamoja na mashindano ya vyuo vya ualimu UMISAVUTA ambao wamekua wakikosa nafasi ya kuendelea kuonesha vipaji vyao baada ya kumaliza masomo," alisema Kibombe.

Aliongeza: "Tunaishukuru kwa dhati kabisa Bodi ya Korosho Tanzania ambayo ndio mdhamini mkuu wa Klabu ya Korosho Queens kwa msimu wa 2023".

Alisema Bodi ya Korosho Tanzania ilitoa jezi, mipira, viatu na kufadhili gharama zote za chakula, malazi na safari za timu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KANE AWANIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imemfanya mshambuliaji wa Tottenham Hotspur ya England, Harry Kane, 29, kuwa kipaumbele chao msimu huu baada ya kuondoka kwa mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, 35. ***(Le Parisien)***

### WALKER ATAKA KUBAKI

MLINZI wa England, Kyle Walker, 33, anataka kubakia Manchester City na yuko kwenye mazungumzo juu ya kuongezewa mkataba, licha ya Bayern Munich kuonesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Mail)***

### SILVA ATAKIWA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva, 28, amepokea ofa ya kujiunga na Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League. ***(Athletic)***

### RASHFORD KUJIFUNGA TENA

MSHAMBULIAJI wa England, Marcus Rashford, 25, yuko mbioni kusaini mkataba mpya wa muda mrefu katika Klabu ya Manchester United. ***(Mail)***

### KAI AIFUNGUA NJIA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Kai Havertz, 24, hana nia ya kusaini mkataba mpya Chelsea, huku mchezaji huyo akinyatiwa na Arsenal. ***(ESPN)***

### ARUHUSIWA KUONDOKA

ARSENAL imempa ruhusu kiungo wa kati wa Ghana, Thomas Partey, mwenye umri wa miaka 30, kutathmini uhamisho wa kwenda Ligi Kuu Saudi Arabia. ***(90 min)***

### PICKFORD KUBAKI EVERTON

GOLIKIPA wa Everton na England, Jordan Pickford, mwenye umri wa miaka 29, amesema atabaki Goodison Park na hajawasiliana na Manchester United. ***(Mail)***

### OSIMHEN KUBAKISHWA

KLABU ya Napoli ina matumaini ya kufikia mkataba na mshambuliaji wao, Victor Osimhen, lakini wamekiri kwamba, watazingatia ofa ya Mnigeria huyo mwenye umri wa miaka 24, msimu huu wa majira ya joto. ***(Metro)***

### GRAVENBERCH NA LIVERPOOL

LIVERPOOL inataka kumsajili kiungo wa Uholanzi, Ryan Gravenberch, mwenye umri wa miaka 21, kutoka Bayern Munich msimu huu wa majira ya joto. ***(Mirror)***


### HAITAKI BUNDESLIGA

KIUNGO wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan, mwenye umri wa miaka 32, amesema wakala wake alitafutwa na Borussia Dortmund, lakini "sina mpango" wa kurudi Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga. ***(Goal)***

### DOHERTY ATAJWA SAUDIA

MLINZI wa zamani wa Tottenham Hotspur na mchezaji wa Kimataifa wa Jamhuri ya Ireland, Matt Doherty, mwenye umri wa miaka 31, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru, anahusishwa na kutakiwa Ligi Kuu Saudi Arabia. ***(Sun)***

## DONDO SOKA
## MAGAZE LAYA




# MBAPPE AWEKA REKODI MPYA NCHINI UFARANSA

**PARIS,** Ufaransa

### ●●● Pia mshambuliaji huyo wa PSG amemfikia nyota wa Norway na Man City, Haaland...

KYLIAN Mbappe ameweka rekodi mpya wakati Ufaransa ikidumisha rekodi yake kwa asilimia 100 kwenye kufuzu kwa euro 2024 Kundi B kwa ushindi wa nyumbani wa bao 1-0 dhidi ya Ugiriki iliyomaliza mchezo na wachezaji 10, Jumatatu.

**Mbappe alifunga penalti kipindi cha pili na kuweka rekodi ya kuwa mfungaji bora wa Ufaransa kwa msimu mmoja akiwa na mabao 54 kwa klabu na taifa, akivunja ile iliyowekwa na Just Fontaine msimu wa 1957-58.**

Pia ilimsaidia fowadi huyo wa Paris Saint-Germain kumfikia mshambuliaji wa Norway na Manchester City, Erling Haaland. Ingawa Haaland alikuwa na nafasi ya kuongeza idadi ya mabao mengi kwa msimu mmoja kama mfungaji bora kati ya wale wanaocheza kwenye ligi tano bora za Ulaya wakati timu yake ya taifa jana, Jumanne ilipocheza na Cyprus.

Matokeo hayo yameiacha Ufaransa kileleni mwa Kundi B ikiwa na pointi 12, sita mbele ya Ugiriki inayoshika nafasi ya pili, ambapo ilimpoteza Konstantinos Mavropanos aliyetolewa kwa kadi nyekundu kipindi cha pili.

"Ulikuwa msimu mrefu kwa wachezaji," alisema kocha wa Ufaransa Didier Deschamps.

"Tulifanya kile tulichohitaji kushinda mchezo huu hata kama tunaweza kujuta hatukupata bao lingine kwa sababu huwezi kujua nini kinaweza kutokea mwishoni mwa mchezo."

Randal Kolo Muani alipata nafasi ya wazi dakika ya 25 kwa mpira wa kichwa kutokana na pasi ya Mbappe, lakini mpira ulitoka nje.

Ilikuja baada ya fursa za awali kwa Mbappe na Kingsley Coman, lakini watatu hao hawakuweza kulenga goli.

Baada ya ushindi wa mabao 3-0 Jumamosi dhidi ya Gibraltar, Ufaransa sasa wamefunga mabao tisa na kutoruhusu nyavu zao kutikiswa katika michezo yao yote minne ya kufuzu.

Septemba 7, mwaka huu watacheza na Ireland nyumbani, huku Ugiriki ikisafiri hadi Uholanzi.

## HABARI MICHEZO

# ARSENAL YAMRUHUSU PARTEY KUONDOKA




**LONDON,** England

ARSENAL wamempa ruhusa kiungo, Thomas Partey, kutathmini uhamisho wa kwenda kucheza kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, kwa mujibu wa 90min.

Saudi Arabia inaingiza fedha kwenye ligi yake, ambayo tayari imeshuhudiwa Cristiano Ronaldo na Karim Benzema wakipeleka maisha yao huko mwaka huu.

Kulikuwa pia na nia ya kumchukua Lionel Messi, lakini ameamua kwenda Marekani, huku wachezaji wengine wengi wakiwamo Hakim Ziyech, Kalidou Koulibaly na Ruben Neves wakitajwa kuelekea huko.

Partey alijiunga na Arsenal kwa uhamisho wa pauni milioni 45 kutoka Atletico Madrid mwaka 2020 na kushiriki katika mechi 33 kati ya 38 za Ligi Kuu msimu uliopita.

Lakini Arsenal wanatafuta kutengeneza kikosi cha vijana cha kutumainiwa na wako tayari kumwachia Partey mwenye umri wa miaka 30, licha ya kurejea Ligi ya Mabingwa Ulaya na ni miaka mitatu tu baada ya kumfanya kuwa mchezaji wa nne ghali zaidi katika historia yao.

90min inaelewa kuwa mpango wa Partey kuelekea Saudi Arabia kwa uhamisho wa kudumu, badala ya kubaki Ulaya, ni kwamba 'Washikabunduki' hao wana matumaini ya kupata faida ya kumuuza kwa zaidi ya paui milioni 45 walizolipa.




# *Guardiola: Nitapambana kumbakisha Gundogan*

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amekiri kuwa yuko tayari kupambana kumbakisha Ilkay Gundogan katika Klabu ya Manchester City zaidi ya msimu huu.

Mkataba wa sasa wa Gundogan katika Klabu ya City unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa Juni hii baada ya msimu wa kihistoria kwa mchezaji huyo na klabu, lakini Barcelona wametoa ofa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ili akacheza kule Camp Nou.

Guardiola hivi majuzi alifichua kwamba Mkurugenzi wa Michezo, Txiki Begiristain, anafanyia kazi mkataba mpya wa mchezaji huyo, lakini licha ya jitihada zao nzuri, 90min inaelewa kuwa Barcelona kwa muda mrefu wamekuwa na uhakika wa kupata huduma yake msimu huu wa majira ya joto.

Barcelona wamempa Gundogan mkataba wa miaka miwili pale Camp Nou, pamoja na chaguo la mwaka mmoja zaidi. Vyanzo vya habari pia vimethibitisha kuwa familia ya mchezaji huyo inataka kuishi Hispania.

Hata hivyo, Guardiola hayuko tayari kukubali kushindwa kwa sasa na aliapa kupigana vita kumzuia nahodha huyo wa City kuondoka.

"Tuna nia ya kuongeza mkataba wake na (Barcelona) pia ina nia," alisema Guardiola katika mashindano ya Gofu ya Puma Legends.

"Natumaini atabaki nasi. Bado tunapigania abaki nasi. Ni mchezaji tunayetaka abaki, na tutafanya kila tuwezalo, lakini tunajua Barca wanamtaka.

Gundogan ni mmoja wa wachezaji kadhaa wa City wanaohusishwa na kuondoka pale kwenye Dimba la Etihad msimu huu wa majira ya joto, huku Bernardo Silva pia akitafuta kuondoka katika klabu hiyo msimu huu.

# Chelsea kuwaachia Ziyech na Koulibaly

**LONDON,** Engand

HAKIM Ziyech anakaribia kukamilisha uhamisho wa kutoka Chelsea kwenda Klabu ya Al-Nassr ya Saudi Arabia, huku mlinzi Kalidou Koulibaly pia akikaribia kuhamia huko Mashariki ya Kati, kwa mujibu wa ESPN.

Chelsea inatazamia kuingiza fedha msimu huu wa majira ya joto, katika kukabiliana na madirisha mawili ya matumizi makubwa na kufadhili biashara zaidi mwaka huu, huku Ziyech na Koulibaly wakiwa miongoni mwa wachezaji kadhaa waliowaweka sokoni.

Mmiliki mwenza wa 'Blues' hao, Todd Boehly, hivi majuzi alikuwa nchini Saudi Arabia kwa mikutano na maofisa kadhaa wa soka, na kupatikana kwa wachezaji hao wa pembeni wa Chelsea ilikuwa miongoni mwa mada za mazungumzo.


Wakuu wa Saudi wamekubaliana na mpango huo haraka na vyanzo vimethibitisha kwamba Ziyech atakuwa mchezaji wa kwanza wa Chelsea kuelekea Mashariki ya Kati msimu huu wa majira ya joto.

Ziyech amekubali mkataba wa miaka mitatu kuungana na Cristiano Ronaldo katika Klabu ya Al-Nassr na hivi karibuni atafanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kuweka bayana kuhusu uhamisho huo.

Kwa Koulibaly, mazungumzo yanaendelea kuhusu kuhamia Al-Hilal. Beki huyo wa kati wa zamani wa Napoli amekataa uhamisho wa mkopo kwenda Serie A ili apate uhamisho wa kudumu kwenda Saudi Arabia.

Makubaliano kuhusu maslahi binafsi yanakaribia kukamilishwa, na mkataba wa miaka mitatu hadi 2026 pia uko mezani kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31.

Kipa Edouard Mendy pia amekubali kusaini mkataba wa miaka mitatu na Al Ahli, ambao sasa wanatafuta makubaliano juu ya ada ya uhamisho na Chelsea. Mkataba unatarajiwa kukamilika baadaye wiki hii.



HABARI MICHEZO

# Bares ajiweka sokoni klabu za Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI baadhi ya klabu za Ligi Kuu zikihaha kutafuta makocha wakuu na wasaidizi, Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Abdallah Mohamed 'Bares', amesema yupo tayari kuifundisha timu yoyote ya Ligi Kuu Tanzania Bara kama atafuatwa na kuelewana maslahi.

Bares aliyeitoa Prisons mkiani na kufanya kuwa timu tishio kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, alisema jana kuwa wala hahitaji kujipigia debe sana kwani watu wote kazi yake wameiona, hivyo yupo tayari kufanya kazi na klabu yoyote.

"Ligi imemalizika, mwenye kuona kazi ya Bares ameiona kama anahitaji mazungumzo mimi niko tayari, watu wa mpira sisi tunaangalia zaidi maslahi na si kitu kingine, pamoja na kwamba bado ni kocha wa Prisons, lakini wapo watu wanaweza kunipa maslahi mazuri zaidi ya haya ninayoyapata, haya ndiyo maisha ya wacheza soka na makocha, milango iko wazi," alisema Bares.

Akiwazungumzia pia mabingwa wa Kombe la Mapinduzi, timu yake ya zamani ya Mlandege, alisema ni kati ya jambo ambalo atabaki analikumbuka hasa kwa uamuzi wake kuacha kuinoa timu ambayo ilikuwa bingwa na mshindi wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar, na kwenda kuinoa Prisons iliyokuwa inashika nafasi ya mwisho kwenye Ligi Kuu Bara.

"Tujipongeze Prisons kwa sababu tumetoka kwenye nafasi mbaya sana, kuna wakati tulikuwa mkiani, tukapanda, inafika wakati mechi za kumalizia ligi hatukuwa miongozi hata mwa timu zilizo kwenye hatari ya kucheza 'play off'', na umekuwa msimu ambao nimeweka kumbukumbu ambayo sitoisahau kwenye soka la Tanzania tangu nilipoanza kufundisha mpira wa miguu, niliichukua timu kwenye wakati mgumu, ilikuwa ni kama nimejivisha mwenyewe mabomu," alisema.



# 'THANK YOU' SASA YAANZA KUANGUKIA NYOTA SIMBA



Mohamed Quattara

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Klabu ya Simba imeanza kupitisha panga kwa wachezaji wake ambao hawatokuwa sehemu ya kikosi msimu ujao, baada ya kutangaza kuachana na beki wa kati Mohamed Quattara na kiungo mkabaji Victor Akpan aliyekuwa akiichezea Ihefu FC kwa mkopo.

Baada ya kutoa mkono wa kwaheri kwa baadhi ya watu wa benchi la ufundi hivi majuzi, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alitanabaisha kuwa itaanza kutangaza wachezaji mmoja mmoja, ambao hawatokuwa nao kuanzia Jumatatu, lakini ilishindikana na jana, Jumanne imeanza kuwapa 'thank you' wakianza na mchezaji huyo.

Kutangazwa kwa wachezaji hao tayari kumefungua mlango wa mfululizo wa klabu hiyo kutangaza wachezaji wengine wengi ambao wataachwa kuelekea msimu ujao wa mashindano kupisha usajili mpya.

"Tulikuwa na matarajio makubwa na Quattara kutokana na uwezo aliokuwa nao kabla ya kujiunga nasi, lakini hali ilikuwa tofauti huku majeraha nayo yakichangia sehemu kubwa," ilieleza taarifa ya Simba jana.

Kuhusu Akban ilieleza: "Baada ya kuwa kwenye kikosi chetu kwa msimu mmoja, Victor Akpan hatakuwa sehemu ya timu yetu ya msimu ujao."

**Hata hivyo, wanakuwa wachezaji wa pili na wa tatu kupewa mkono wa kwaheri baada ya Augustine Okrah raia wa Ghana, ambaye ndiye alikuwa wa kwanza kuachwa kabla hata ligi haijamalizika.**

Majuzi, klabu hiyo ilitangaza kuwaacha kocha wa magolikipa, Chlouha Zakaria, Kelvin Mandla ambaye ni kocha wa viungo, mtaalamu wa viungo, Fareed Cassim na Kocha Mkuu wa timu ya wanawake, Simba Queens, Charles Lukula. Akpan raia wa Nigeria, alisajiliwa na klabu hiyo Julai mwaka jana kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Coastal Union.

Hata hivyo, alikaa nusu msimu tu huku akishindwa kuonyesha kiwango kilichowashawishi makocha Zolan Maki aliyekuwapo wakati huo, Juma Mgunda mwenyewe ambaye alikuwa naye Coastal Union na hata Robertinho Oliveira aliyejiunga Novemba mwaka jana, hivyo haikushangaza alipopelekwa Ihefu FC kwa mkopo Januari mwaka huu.

Ukiacha Akpan, wachezaji wengine ambao wanatajwa kuwa miongoni ya walioanza kupewa neno 'thank you' ni pamoja na Ismael Sawadogo, Gadiel Michael, Habib Kyombo, Jonas Mkude, Nassor Kapama na wengineo.

Simba imedhamiria kupitisha panga la nguvu baada ya kutokuwa na taji lolote kwa misimu miwili mfululizo.

# *Mayele sasa aanika hatima yake Yanga*

INATOKA UKURASA 24

mwa viongozi wa timu yake hiyo zikihitaji huduma yake.

Alisema baada ya kumaliza majukumu ya timu ya Taifa anatarajia kukutana na viongozi wa timu yake kwa ajili ya mazungumzo kuhusu ofa za klabu zilizomhitaji.

"Watu wanasubiri 'Thank You' ya kwangu ila hatima yangu ipo chini ya viongozi wa Yanga, nilikuwa na majukumu na timu ya taifa, lakini sasa narudi Tanzania maana familia yangu iko huko, najua watu wengi wanasubiri neno hilo ambalo kwa sasa limekuwa maarufu.

"Ofa zipo nitakutana na tutazungumza na viongozi wangu juu ya hatima yangu kama kusalia ndani ya kikosi au la," alisema Mshambuliaji huyo.

Aliongeza kuwa baada ya kumalizana na kujua hatima yake, ataenda visiwani Zanzibar kumsapoti mchezaji mwenzake wa zamani wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', ambaye ameandaa mechi kwa ajili ya kuwasaidia kinamama wajawazito.

"Nitaenda visiwani Zanzibar kucheza mechi Juni 24, mwaka huu katika Uwanja wa Mao Zedong na baada ya hapo nitaelekea Morogoro kwenye mechi ya hisani Juni 30, mwaka huu mchezo uliondaliwa na Shomari Kibwana na Dickson Job," alisema Mayele huku akitania na wachezaji wenzake hao kwa kudai kuwa atacheza timu ya yule atakayempa pesa nyingi kati ya Kibwana na Job kwa sababu anapenda sana pesa.

# Mgunda anukia

INATOKA UKURASA 24

na sasa niko Tanga baada ya mapumziko na muda utakapofika nitarejea kwenye majukumu yangu Simba," alisema kocha huyo.

Nipashe lilimtafuta Meneja wa timu ya Simba Queens, Selemani Makanya, ambaye alisema hata yeye amekuwa akizisikia tetesi za Mgunda kuwa sehemu ya benchi la ufundi la timu hiyo kuchukua mikoba ya Lukula, lakini hajapewa taarifa rasmi.

"Bado sijapewa taarifa zozote kuhusu kocha mkuu maana ninachojua uongozi uko kwenye mchakato, kuhusu Mgunda hata mimi nimesikia hivyo, kuwa anakuja kwenye timu yetu ila bado sina taarifa kamili na ninaimani viongozi wanajua nini wanafanya kwenye maboresho ya mabenchi ya ufundi ikiwamo la kwetu la Simba Queens," alisema meneja huyo.

# Michezo

Jumatano Juni 21, 2023

Nipashe




## Arsenal yamruhusu Partey kuondoka

UKURASA 22

TANGULIA NAJA...




Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akipishana na aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi, katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana baada ya kutua akitokea kwenye majukumu ya Timu ya Taifa, DR Congo, huku Nabi akiondoka rasmi nchini baada ya kumaliza mkataba wake na klabu hiyo na kukataa kuongeza. Wengine ni mke wa Mayele na wanawe waliofika kumlaki uwanjani hapo na kumkabidhi mumewe kiatu cha ufungaji bora alichotwaa msimu huu. **PICHA: NA MPIGAPICHA WETU**

## Mgunda anukia Simba Queens

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Simba ukiendelea kuhakikisha unaboresha na kuongeza nguvu ya benchi la ufundi la timu hiyo, inadaiwa Kocha Msaidizi wa kikosi hicho, Juma Mgunda, anatarajiwa kwenda kuchukua nafasi ya Charles Lukula aliyekuwa akikinoa kikosi cha Simba Queens.

Simba Queen inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, ambayo msimu huu imemaliza nafasi ya pili na kushindwa kutetea taji lao la ubingwa, hivi karibuni uongozi wa klabu hiyo ulitangaza kuachana na kocha Lukula pamoja na makocha wengine wa timu ya wanaume wakiwamo kocha wa makipa , Chlouha Zakaria, wa viungo, Kelvin Mandla na mchua misuli, Fareed Cassiem.

Taarifa kutoka chanzo chetu ndani ya uongozi wa Simba, zimeeleza kuwa Mgunda ataendelea kusalia ndani ya Wekundu wa Msimbazi hao kwa kupewa jukumu la kukinoa kikosi cha timu ya wanawake kwa msimu ujao.

Zilisema hiyo ndiyo mipango ya Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo baada ya kukutana wiki iliyopita na huku kocha wa viungo wa timu ya wanaume, Simba akitajwa kuwa atakuwa ni yule wa Vipers FC ya Uganda, Raia wa Rwanda, Hategekimana Corneille, ambaye atatua kuchua nafasi ya Kelvin.

Kwa upande wa Mgunda alisema bado yupo sana Simba na sasa yuko kwenye mapumziko baada ya msimu wa 2022/23 kumalizika hivi karibuni.

"Bado ni mfanyakazi wa Simba

INAENDELEA UKURASA 23

# Mayele aanika hatima yake

**Na Saada Akida**

## Asema anatambua wengi wanasubiri neno 'Thank You' na kwamba tayari amepata ofa...

HUKU akiendelea kuhusishwa na klabu kadhaa nje ya nchi zinazohitaji huduma yake kuelekea msimu mpya wa 2023/24, mshambuliaji wa Yanga raia wa DR Congo, Fiston Mayele, ameweka hatima yake ya kuendelea kusalia ndani ya kikosi cha timu hiyo kwa msimu wa mashindano wa 2023/24 kuwa upo mikononi mwa viongozi wa klabu hiyo.

Mayele ameibuka kuwa miongoni mwa wa washambuliaji bora kwa sasa barani Afrika na ameweka rekodi nyingine ya kuwa mchezaji ambaye amefunga katika kila mashindano aliyocheza msimu huu kuanzia ngazi ya klabu hadi timu ya taifa.

Mshambuliaji huyo amekuwa na kiwango kizuri kwa msimu huu kwa kutwaa Kiatu cha Ufungaji Bora Ligi Kuu Bara akishirikiana na kiungo wa Simba, Saido Ntibazonkiza baada ya kina mmoja kuweka nyavuni mabao 17, lakini Mkongomani huyo pia akionyesha ubora pia kwa kuwa kinara wa ufungaji kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika akimaliza na mabao saba.

**Kiwango hicho kimemfanya kuhusishwa na kutakiwa na klabu mbalimbali ikiwamo Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini ambayo Kocha wake, Nasreddine Nabi, huku timu nyingine inayohitaji huduma yake ikitajwa kuwa ni Mamelodi Sundowns ya nchini humo.**

Akizungumza na Nipashe jana, Mayele alisema ana mkataba wa mwaka mmoja umesalia ndani ya klabu yake hiyo na tayari amepata ofa nyingi ambazo ziko mezani

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >